Jumanne Februari 9, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580486

www.ippmedia.com

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Nipashe

TESA

Jumanne Februari 9, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 13

Ndivyo Magereza inavyoliokoa taifa na mbegu 'zinazoogopwa'

Ukurasa 14

Mkoa ulivyounda mabaraza vijiji, kukomesha ubakaji, ndoa utotoni

ELIMU

NA SABATO KASIKA

KHE INASHAGAZA!...

Madawati yabaki tupu darasani, kisa mabinti wapewa ujauzito

WANAFUNZI zaidi ya 20 waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu wilayani Serengeti katika mkoa wa Mara, wamebainika kuwa ni wajawazito hivyo hawakuanza masomo ya sekondari Januari 2021, hali inayopunguza wasichana madarasani na kuwarudisha nyuma kitaaluma.

Ni kwa mujibu wa maelezo ya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu, anayoyatoa kwa wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wilaya, akisema tatizo hilo ni kubwa na linaathiri maendeleo ya elimu kwa wasichana.

"Tayari watuhumiwa wanne wameshakamatwa kuhusika na matukio hayo ambayo ni kikwazo kwa maendeleo ya elimu ya mabinti, inatakiwa kuanzia sasa kila mmoja ...

Serengeti inatajwa kufanya vizuri, lakini inaharibiwa na tatizo la mimba ambalo linakwamisha maendeleo ya elimu kwa wanafunzi wa kike, hivyo juhudi za kulimaliza zinatakiwa kufanywa na wadau wote na kuwataka wazazi, walezi na viongozi wa maeneo husika kuwa mstari wa mbele kukemea ukatili huo unaofanywa na mafataki ili usawa wa kijinsia katika elimu uonekane.

KIKWAZO KINGINE

Hadi Desemba mwaka jana, watoto wa kike 55 wakiwamo wanafunzi, walikuwa wamehifadhiwa nyumba salama ya mjini Mugumu ya Hope for Girls baada ya kukwepa ukeketaji unaofanywa nyumbani kwao, anasema Mkurugenzi wa Hope for Girls, Rhobi Samwelly na kuongeza kuwa tayari wamesharudishwa kwa wazazi wao ili waendelee na masomo, baada ya kuhakikishiwa kuwa hawatakeketwa.

"Hope for Girls kwa kushirikiana na wadau wa uetetezi wa mtoto wa kike wakiwamo Dawati la Jinsia na Ustawi wa Jamii tumewarudisha kwa wazazi wao kwa masharti," anasema Rhobi na kuyataja kuwa ni pamoja na wazazi kujaza fomu maalum wakikiri kutojihusisha tena na vitendo hivyo kwa watoto wao na ...

UKURASA 11

**TABOA** yalalamikia mfumo wa mtandao kukatisha tiketi



UKURASA 3

**RIPOTI MAALUM-2**

Maajabu ya watoto wenye saratani

UKURASA 19

MAHOJIANO MAALUM

# Mwinyi: Ajira nyingi zinakuja

**AFUNGUKA** umuhimu Maalim Seif kuungana naye, uchumi wa bluu na vita kuukabili ubadhirifu...*Endelea Uk. 4*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.



# Bunge laishauri serikali kupaa kwa deni la Taifa

**BAJETI** ya 2021/22 kutumia tril. 36.26/- *Endelea Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### TANZANIA NA AFRIKA KUSINI ZAWASILISHA OMBI MAALUM AU

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Jamhuri ya Afrika Kusini zimewasilisha ombi maalumu kwa Umoja wa Afrika (AU) kuzitambua rasmi njia zilizotumika na wapigania uhuru kutoka Dar es Salaam kupitia nchi mbalimbali Kusini mwa Bara la Afrika hadi Namibia kuwa urithi wa kimataifa...

UKURASA WA 5

### MFUMUKO WA BEI WAONGEZEKA

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Januari 2021, umeongezeka kutoka asilimia 3.2 kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2020, hadi asilimia 3.5 kwa mwaka ulioishia mwezi Januari...

### MBUNGE ATAKA KUSITISHWA TOZO ZA UTALII ZA TANAPA

UKURASA 3

**MICHEZO** KAZE APIKA MABAO YA FISTON, SARPONG YANGA UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Bunge laishauri serikali deni la Taifa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

DENI la Taifa limefikia Sh. trilioni 59 hadi kufikia Desemba mwaka jana, ikilinganishwa na Sh. trilioni 54.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 7.6, huku Bunge likitoa ushauri liwe himilivu.

Kati ya kiasi hicho, deni la ndani limefikia Sh. trilioni 16.2 na deni la nje Sh. trilioni 42.8. Ongezeko la deni limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Pamoja na kwamba deni hilo ni himilivu kwa viashiria vyote muhimu, serikali imeshauriwa ione haja ya kujipima uhimilivu wake, kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani, kwa pato la Taifa ambacho kwenye mpango hakijaripotiwa.

Hayo yalibainishwa na Sillo Baran, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, alipokuwa akiwasilisha taarifa kuhusu tathmini ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano (2016/17-2020/21), mapendekezo ya Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/22-2025/26) na Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka wa fedha 2021/22, na kusema wanashauri hilo kwa sababu deni la taifa uhudumiwa na makusanyo ya ndani na ni malipo ya lazima katika matumizi ya serikali.

"Vilevile kamati inaishauri serikali kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa credit rating (kiwango cha mkopo) ili kuiwezesha serikali kupata mikopo nafuu na kwa urahisi," alisema mwenyekiti huyo.

Alisema kwamba kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Desemba 2020, deni ni himilivu kwa vigezo vyote vya kimataifa na hivyo nchi ina uwezo wa kukopa ndani na nje, na kulipa mikopo hiyo bila kuwa na athari hasi kwenye ukuaji wa uchumi.

Katika maoni ya jumla ya kamati hiyo ya bajeti, serikali imeshauriwa kutafuta njia ya kupunguza kukopa katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya bajeti kwa kupitia dhamana ya serikali na hati fungani.

Badala yake, serikali ijikite zaidi katika kuongeza udhamini wa wakopaji wadogo (credit gurantee schemes) pamoja na kuongeza matumizi ya mikopo inayojidhamini yenyewe (lease finance).

Vilevile, serikali iangalie uwezekano wa kufungua zaidi soko la mitaji (liberization of capital market) ili kupunguza athari za serikali kukopa kwenye soko la ndani.

Akiwawilisha bungeni mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, Waziri wa Sheria na Katiba, Dk. Mwiguli Nchemba, alisema ongezeko la deni hilo limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji.



Mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22, yaliwasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba.

Yamo pia malimbikizo ya riba ya deni la nje, hususani nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris Club ambazo serikali inaendelea kujadiliana nazo.

Kwa mujibu wa Dk. Nchemba, tathmini ya uhimilivu wa deni imeonyesha kuwa deni la serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia ukomo unaokubalika kimataifa kwa viashiria vyote muhimu.

"Kwa mwaka 2020/21, thamani ya sasa ya deni la serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.9, ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; thamani ya sasa ya deni la nje, kwa pato la taifa ni asilimia 17.3, ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; na thamani ya sasa ya deni la nje, kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2, ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240," alifafanua Waziri Nchemba.

Aidha, alieleza kuwa ulipaji wa deni la nje, kwa mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 13.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23.

## Bajeti mwaka wa fedha 2021/2022 ni Tril. 36.26/-

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2021/22 inatarajiwa kukusanya na kutumia Sh. trilioni 36.26, sawa na ongezeko la asilimia 4.0 ya bajeti ya mwaka 2020/21 ya Sh. trilioni 34.88.

Maeneo ya kipaumbele mwaka huu ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Jana, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha bungeni mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango, bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22, alisema serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya Sh. trilioni 36.26.

Mwigulu aliwasilisha mapendekezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, na kusema: "Ongezeko hilo linatokana na mahitaji ya mfuko mkuu wa serikali ikijumuisha malipo ya deni la serikali, mahitaji ya upandishwaji wa madaraja ya watumishi na ajira mpya.

"Na mahitaji ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)."

Kupitia mpango wa maendeleo wa miaka mitatu, serikali imejikita zaidi katika kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta za viwanda, biashara na uwekezaji.

Kwenye mapendekezo hayo, maeneo yaliyozingatiwa katika mpango huo ni kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa mwaka, mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri kuongezeka, mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja, akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji na sekta binafsi kuzalisha ajira mpya zipatazo milioni nane.

Aidha, Dk. Mwigulu aliwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano wa mwaka 2021/22-2025/26.

Akizungumzia mpango wa kitaifa wa 2021/22 pamoja na mwongozo wa bajeti ya mwaka huo wa fedha, Waziri Mwigulu, alisema katika eneo la kuchochea uchumi shindani na shirikishi, litajumuisha miradi itakayojikita katika kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa na kuimarisha utulivu wa uchumi.

"Pia litajikita katika kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuimarisha uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje na kuendeleza miundombinu na huduma katika maeneo ya reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), nishati, bandari na viwanja vya ndege.

Vile vile, alisema katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani eneo hilo litajumuisha kuendeleza viwanda vya uzalishaji wa dawa kwa matumizi ya binadamu, miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini.

Katika kukuza biashara, alibainisha kuwa eneo hilo litajumuisha programu za kuimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko ya kikanda na kimataifa.

Kuhusu kuchochea maendeleo ya watu, alisema eneo hilo litajumuisha utekekelezaji inaojikita katika kuboresha maisha ya watu ikiwamo kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote; afya na ustawi wa jamii, kinga ya jamii, huduma za maji na usafi wa mazingira; mipango miji, na nyumba na maendeleo ya makazi. Alisema pia eneo lingine la kuendeleza rasilimali watu litajumuisha programu na mikakati inayolenga kuendeleza ujuzi wa rasilimali watu nchini, kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwamo kuwawezesha vijana kujiajiri.

Alisema pia mpango na mwongozo huo, utajumuisha miradi ya kielelezo inayoendelea ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kuwa na matokeo makubwa na ya haraka katika uchumi.

### MIRADI YA KIELELEZO

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere - MW 2,115, kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa, makaa ya mawe - Mchuchuma na Chuma –Liganga, ikijumuisha ujenzi wa reli kiwango cha standard gauge kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga.

Miradi mingine ni bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), mradi wa kuchakata gesi asilia kuwa kimiminika (LNG) – Lindi, mradi wa kufua umeme wa maji wa Rufiji (MW 358), mradi wa kufua umeme wa maji wa Rumakali (MW 222); uchimbaji wa madini ya nickel; ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za juu (interchange) za daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza.

### WASHIRIKA WA MAENDELEO

"Washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia Sh. trilioni 2.89 sawa na asilimia 7.9 ya bajeti yote mwaka 2021/22. Katika kipindi hicho, serikali inatarajia kukopa Sh. trilioni 4.99 kutoka soko la ndani," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Mwigulu, alisisitiza kuwa kati ya kiasi hicho, Sh. trilioni 3.15 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za serikali zinazoiva, na kiasi cha Sh. trilioni 1.84 ni sawa na asilimia 1.1 ya pato la taifa ni mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo," alisema.

Aidha, alisema mikopo ya masharti ya kibiashara kutoka nje inatarajiwa kuwa Sh. trilioni 2.35 mwaka 2021/22.

"Mheshimiwa Spika, matumizi ya serikali yanakadiriwa kufikia Sh. trilioni 36.26, ambapo Sh. trilioni 23.0 ni matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 13.26 ni matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 37 ya bajeti yote," alifafanua.

Alieleza kuwa matumizi ya kawaida yana jumuisha mishahara Sh. trilioni 8.15 (sawa na asilimia 31.3 ya makadirio ya mapato ya ndani), malipo ya riba na mtaji kwa deni la ndani, na nje Sh. trilioni 8.88 na matumizi mengineyo Sh. trilioni 5.97.

HABARI KITAIFA

## TABOA yalalamikia mfumo wa mtandao kukatisha tiketi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), kimetoa kilio kuhusu mfumo wa tiketi mtandao, kikitoa maazimio manne yanayopaswa kufanyiwa kazi na Mamlaka ya Udhibiti Usafirishaji Ardhini (LATRA).

Msemaji wa TABOA, Thabit Mfaume, alisema Kamati ya Utendaji TABOA ilikutana kujadili kwa kina matatizo wanayokumbana nayo kuhusu mfumo wa tiketi mtandao.

Alisema wajumbe wa kamati walieleza kuwa mfumo huo unachangamoto ambazo zinapaswa kurekebishwa haraka na LATRA, kwamba hawaukatai.

Mfaume alisema wajumbe walitoa maazimio manne ikiwamo LATRA kuacha kupiga faini wamiliki wa mabasi kutokana na kutokutumia mfumo au kushindwa kutumia mfumo.

Alisema, azimio la pili ni suala la kuweka 'floot' (mtaji) kwa asilimia mia haiwezekani kwa sababu ni mzigo kwa wamiliki wa mabasi.

"Itamlazimu mmiliki kuwa na mitaji miwili na inaongeza gharama za uendeshaji, pia wamiliki tunapendekeza tuweke asilimia mbili tu kwenye mashine ili serikali na wazabuni wachukue makato yao," alisema Mfaume.

Alisema azimio la tatu ni mfumo huo hauna uhakika kwa sababu wamiliki wa mabasi wanalalamika kupoteza pesa.

"Wamiliki wa mabasi wakiweka pesa kwenye mashine na baada ya floot kwisha pesa hazionekani benki wala kwenye floot, hivyo mfumo siyo salama kwa pesa za wamiliki," alisema Mfaume.

Mfaume alisema azimio la nne ni mfumo kuhakikiwa, kuwe na uhakika, ufanisi, kwa sababu wamiliki wa mabasi wanapigwa faini wakati hawajasababisha kutokea kwa ubovu wa mfumo.

"Kamati imetoa rai kwa LATRA kuchukua changamoto hizo na kuzifanyia kazi kwani kama hazitapatiwa ufumbuzi kwa haraka wasafirishaji watashindwa kuendelea kutoa huduma."

Naye Meneja wa mabasi ya Al-Saedy, Mwishehe Said, alisema: "Leo ni siku ya nane sijarudishiwa pesa zangu, nimejaribu kufuatilia na kuuliza lakini sijafanikiwa. LATRA wanazuia gari pasipo kuuliza tatizo."

# Serikali yaombwa kusitisha tozo za utalii

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

MBUNGE wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, ameiomba serikali kusitisha tozo za utalii kwa hifadhi zilizo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) zilizotangazwa kuanza kutozwa Julai mwaka 2021, kutokana na sekta ya utalii nchini kuathiriwa na ugonjwa wa corona.

Ongezeko hilo la tozo limezilenga hifadhi za taifa nne ambazo ni Ziwa Manyara, Serengeti, Tarangire na Arusha kwa kipindi cha msimu wa juu wa utalii nchini na kuacha tozo za sasa ambazo zitaendelea kutumika kwa msimu wa chini wa utalii.

Akiuliza swali la nyongeza jana bungeni, Gambo alisema sekta ya utalii kwa Mkoa wa Arusha na nchi nzima imeathiriwa sana ambapo watu wamekosa ajira, madereva wamekosa ajira, waongoza watalii wamekosa ajira, wafanyakazi wa mahoteli wamepunguzwa kazi.

"Kwa ukanda wa Afrika Mashariki nchi nyingi zimepunguza tozo katika kipindi hichi, kwa mfano Kenya kwenye hifadhi ya Nairobi wamepunguza tozo kutoka Dola za Marekani 43,000 hadi 35,000, Rwanda wamepunguza kutoka Dola za Marekani 1500 hadi 500, Uganda wamepunguza kutoka Dola la Marekani 700 hadi 500," alisema.

Aliiomba Wizara ya Maliasili na Utalii iangalie athari za ugonjwa wa corona kwenye masuala ya ajira na mengine.

"Wizara ina mpango gani kuipa ahueni sekta ya utalii ili kunusuru tatizo kubwa ya ajira ambayo imewaathiri wananchi wa Mkoa wa Arusha," alihoji.

Akijibu maswali ya Mbunge huyo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema wakati wafanyabiashara ya utalii wakiishinikiza serikali kuacha tozo zikiwa za chini sana, wenyewe wamekuwa wakiwatoza watalii tozo za juu ambazo hawataki kuziweka wazi kwa serikali.

"Usiri wa tozo za kampuni binafsi unainyima serikali taarifa za msingi za kuona uzito wa hoja yao, naomba kutoa rai kwamba suala la corona lisitumike kuinyima serikali mapato ambayo yanasaidia kukuza uchumi wa nchi," alisema.

Alisisitiza pamoja na shinikizo la kupunguza tozo, sekta binafsi haijawasilisha takwimu zozote serikalini za kuthibitisha kuongezeka kwa idadi ya wageni waliofuta safari zao kuja nchini kutokana na ongezeko la tozo.

Alisema serikali imeongeza tozo hizo zitaendelea kutumika kwa vipindi vyote visivyo vya utalii wa juu tu na lengo la kuwa na tozo za vipindi hivyo viwili ni kuwavutia watalii wengi zaidi kutembelea vivutio hasa kipindi cha msimu wa chini wa utalii.

Aidha, alisema viwango vilivyorejewa kwa baadhi ya hifadhi vililenga kuongeza idadi ya watalii kwenye hifadhi ambazo zimekuwa zikipata watalii wachache hasa za Kusini, Mashariki na Kaskazini-Magharibi.

"Tozo ya kuingilia Hifadhi ya Serengeti mwezi Julai, mwaka huu, itaongezeka kutoka Dola za Marekani 60 hadi 70, na gharama za camping zitaongezeka kwa Dola za Marekani 10 kutoka 50 hadi 60, huku kwa Hifadhi za Manyara, Tarangire na Arusha gharama za kuingia zitaongezeka kutoka Dola za Marekani 45 hadi 50 huku gharama za camping zitakuwa Dola za Marekani 60 kutoka 50," alisema.

Hata hivyo, alisema viwango hivyo ni vidogo sana ikilinganishwa na viwango ambavyo kampuni za utalii zinatoza kwa watalii hao.

"Kwa mfano, 'package' ya kiwango cha chini ya utalii kwa siku tano inayojumuisha kutalii hifadhi za Arusha, Manyara, Serengeti na Ngorongoro huuzwa kwa wastani wa USD 2,500 kwa mtalii mmoja. Katika "Package" hiyo, jumla ya tozo kwa viwango vya sasa ni USD 172 tu, lakini hata pale kampuni za utalii zinapotoza zaidi ya USD 5,000 kwa "package" kama hiyo, TANAPA hupata kiwango hicho hicho cha USD 172,"alisema.



Baadhi ya waliokuwa wafanyakazi wa Hoteli ya Naura Springs na Impala, wakimsikiliza Ofisa Kazi Mkoa wa Arusha, Emmanuel Mweta, akiwapa mrejesho baada ya Mahakama Kuu Arusha kutoa hukumu kwa viwanja vinne vya hoteli hiyo kupigwa mnada, ili kufidia madai yao. **PICHA: DANIEL SABUNI**


LAS VEGAS CASINO

**EMPLOYMENT OPPORTUNITY**

We are inviting applications for experienced:

**ELECTRICIAN, ELECTRONIC TECHNICIAN & IT ADMINISTRATOR**

***Qualification:***

Education of not less than form IV and above, with good knowledge of English.

Should have acquired training from a recognized institution Applicant should have minimum two years' experience.

***General, Requirements:***

If you feel you are a right candidate for this position, kindly submit your application with:

- Detailed C.V.
- Photocopies of academic certificate
- NIDA
- Two passport size photos
- Names of two referees with their contactts.

All applications should be addressed to 'Casino Manager' and handed to the Reception desk between 9:00 am and 4:00 pm at:

Las Vegas Casino, Ali Hassan Mwinyi Road, Upanga, not later than 11/02/2021



**GSP AUCTION MART**

P.o.Box 31088 Dar es Salaam
Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892
Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31
Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

**KUMB No. TATA/2020/DM/018**

GSP AUCTION MART Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Ijumaa tarehe 19/02/2020 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T289DNT | DAR ES SALAAM |
| ABDALLAH KIBWANA KIBWANA | LP909 BUS | T810DMU | DAR ES SALAAM |
| NORBERT JACOB MAGENI | LP909 BUS | T423DQH | MWANZA |
| ABADALLAH RAJABU TERRY | LPO 10.2T/52 | T323DME | DAR ES SALAAM |
| ABADALLAH RAJABU TERRY | LPO 10.2T/52 | T120DMK | DAR ES SALAAM |
| KAJORE OWIGO KITUGE | LPO 10.2T/52 | T430DQA | MWANZA |
| FRED MALI KAZI | XENON | T449DTV | MWANZA |
| BASHIR LEONI MSIMBE | LP 909 BUS | T163 DNT | DAR ES SALAAM |
| BASHIR LEONI MSIMBE | LP 909 BUS | T164DNT | DAR ES SALAAM |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:
GSP AUCTION MART PO BOX 310088
DAE ESSALAAM.
+255 654 922 892, +255 687 638 679**

## MAHOJIANO MAALUM

# Mwinyi: Ajira nyingi zinakuja

- Afunguka umuhimu Maalim Seif kuungana naye
- Uchumi wa bluu, vita kuukabili ubadhirifu...



**Na Sanula Athanas,** ZANZIBAR

SERIKALI mpya ya awamu ya nane Zanzibar, leo inahesabu siku ya 100 kazini. Rais Hussein Ali Mwinyi anafafanua mwelekeo wa utendaji wa kiserikali.

Wanahabari chini ya kivuli cha familia ya IPP, walipata fursa ya kudodosa mwelekeo huo katika mazungumzo maalum na kiongozi huyo visiwani hapa wiki iliyopita.

Katika mazungumzo hayo, pamoja na mambo mengine, Dk. Mwinyi alibainisha namna serikali yake inavyojipanga kutatua tatizo la ajira nchini, akidokeza mipango iliyopo inajumuisha kuajiri watumishi mapya, hasa katika kada za afya na elimu ambazo zina uhaba mkubwa.

Mbali na kuajiri watumishi wapya, Dk. Mwinyi alisema serikali yake iko katika mkakati wa kuwawezesha vijana na wajasiriamali wengine kimitaji, huku akiona fursa nyingine kubwa ya ajira kupitia miradi mikubwa ambayo serikali yake imepanga kuifanya, ukiwamo ujenzi wa bandari ya kisasa na uwekezaji mkubwa katika uvuvi wa Bahari Kuu na uchumi wa bluu kwa upana wake.

Rais Mwinyi pia aligusia maridhiano visiwani Zanzibar, akipongeza mafanikio yaliyopatikana kutokana na Chama cha ACT-Wazalendo kukubali kuungana naye kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Fuatilia sehemu ya mazungumzo ya Rais Mwinyi na wanahabari wa vyombo vya habari vya IPP:

**SWALI: Ni siku 100 tangu ulipoingia madarakani. Mambo yakoje hapa Zanzibar?**

**RAIS MWINYI:** Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa na amani na kutuwezesha kuwa na umoja. Na kweli tunaweza kusema kwamba mambo ni mazuri hapa Zanzibar.

Ni mazuri kwa maana kwamba amani tunayo, wananchi kwa sasa ni 'wamoja' na kwa maana hiyo, mazingira ya kuendelea kuleta maendeleo kwa wananchi wote. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tunafarijika hali ya kimaisha kwa wananchi wetu ni nzuri.

**SWALI: Uliahidi mambo mengi kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka jana. Kipi kimefanyika mpaka sasa katika kutimiza ahadi hizo?**

**RAIS MWINYI:** Kwa kweli ni mapema kusema sasa mambo ambayo tumetimiza, lakini kwa ufupi tu niseme kwamba la kwanza tulizungumza sana suala la amani. Na tunamshukuru Mungu kwa sasa amani tunayo. Tuliwaahidi kuwaunganisha Wazanzibar, wawe wamoja.

Ninashukuru kwamba tumeunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Na kwa maana hiyo, zile kasoro zetu na chuki baina ya watu zimepungua sana na tunaelekea katika umoja wa watu.

Hayo ni mafanikio makubwa sana kwa sababu tumetengeneza mazingira mazuri ya kufanya kazi na kuwajibika ili tupate maendeleo.

Vilevile, nimechukua hatua madhubuti dhidi ya ubadhirifu, wizi wa mali za serikali na rushwa. Na nimeanza kuona matokeo. Sasa watu wanaogopa mali za serikali, ninaona kabisa makusanyo yameanza kuongezeka maeneo mbalimbali. Hizi ni dalili tu maana ndiyo kwanza kazi imeanza. Nina uhakika huko mbele, tutakaa vizuri zaidi.

**SWALI: Hali ya afya hapa visiwani Zanzibar ikoje hasa?**

**RAIS MWINYI:** Bado tuna changamoto nyingi katika Sekta ya Afya ikiwamo miundombinu, bado hatuna miundombinu ya kutosha na vifaa tiba bado tuna upungufu kwenye hospitali nyingi. Pia, kuna tatizo la upungufu wa rasilimali watu; hawatoshi na hao wachache waliopo, pengine hawana utaalamu unaotakiwa.

Vilevile, suala zima la kugharamia huduma za afya bado ni tatizo kwa sababu bado hatuna bima ya afya hapa Zanzibar. Yote haya ni changamoto.

Kuna mafanikio pia. Mfano, Zanzibar imefanikiwa kuuondoa ugonjwa wa malaria. Ni mafanikio makubwa. Tumepiga hatua kubwa sana kwenye ugonjwa wa Ukimwi na kadhalika, magonjwa yale yanayoambukizwa, kipindupindu sasa imebaki historia.

Lakini, hoja ya msingi ni kwamba bado kuna changamoto ambazo tunahitaji kuzifanyia kazi na wadau walituonyesha kwamba tukifanya moja, mbili, tatu, tunaweza kupata mafanikio na ndiyo mpango wa serikali tunakoelekea.

**SWALI: Ni hatua zipi zinachukuliwa na serikali yako kuvitatua vikwazo hivi?**

**RAIS MWINYI:** Kwanza ni kuwa na mipango mizuri. Unapotaka kurekebisha mambo, lazima mipango ikae sawa na ipangiwe bajeti. Kwa mfano, miundombinu tunahitaji Hospitali ya Taifa, tunahitaja hospitali katika ngazi za mikoa na wilaya na kule chini pia.

Je, itatugharimu kiasi gani na hayo majengo yawe ya aina gani? Hayo yote yakiwekwa vizuri, tutajipanga katika bajeti zetu na katika mikopo tutakayochukua kutatua changamoto za miundombinu, lakini hayo mengine ya rasilimali watu na vifaa tiba. Ninafikiri mipango ndiyo kitu cha kuanzia.

**SWALI: Uhaba wa ajira ni tatizo si tu kwa Zanzibar, bali nchi mbalimbali duniani. Serikali yako ina mkakati upi kukabiliana na tatizo hili?**

**RAIS MWINYI:** Ni kweli tuna tatizo kubwa la ajira, siyo kwenye Sekta ya Afya peke yake, bali sekta karibu zote. Upande wa elimu, tuna upungufu mkubwa wa walimu wa Hisabati na Sayansi, madaktari bingwa wamekuwa wachache katika Sekta ya Afya na kadhalika.

Upo mpango wa kuwafundisha. Tunatoa ufadhili wa masomo katika taasisi za serikali na kimataifa pia wanatusaidia sana. Tuna chuo chetu hapa cha SUZA ambacho sasa kinafundisha madaktari. Baada ya muda si mrefu, tutakuwa na madaktari wa kutosha.

Hoja kubwa hapa ni uwezo wa serikali kuajiri na kuwalipa vizuri hao watumishi, jambo ambalo tunalitazama kwa upana wake kwamba, tutawezaje kuajiri na kuwalipa vizuri ili kuwahudumia wananchi?

Kuhusu ajira kwa vijana, kipindi cha kampeni vijana wengi walikuwa na kilio kwamba tatizo lao kubwa ni ukosefu wa ajira na mimi niliwaahidi tutafanya kila linalowezekana kutengeneza ajira mpya nyingi. Ilani yetu ya uchaguzi ilizungumzia ajira 300,000 katika miaka hiyo mitano ambayo ni kazi kubwa.

Ajira zimegawanyika katika makundi matatu; kuna ajira za serikali, kuna ajira za kuajiri wao wenyewe na ajira za sekta binafsi.

Kwa uchumi mpya tunaojaribu kuujenga, tutakuwa na ajira nyingi; kwenye ujenzi wa bandari, kwenye ujenzi wa viwanda, kwenye mambo mbalimbali tutakayoyafanya yataleta ajira kwa vijana.

Upande wa pili katika kujiari, ni muhimu sisi serikali tuwape mafunzo ya kuwawezesha kuajiri wao wenyewe. Kwa mfano, kozi za ufundi, ujenzi.

Ni vyema tuhakikishe tunawapa mafunzo katika vyuo vya ufundi, ili waajirike katika sekta binafsi na wengine wajiajiri wao wenyewe kwa kuwasaidia mitaji na mikopo, jambo ambalo lipo katika mipango ya serikali.

**SWALI: Uchumi wa bluu ni dhana pana ambayo inahitaji uwekezaji wa fedha nyingi. Mpaka sasa serikali yako imefanya nini katika kutimiza azma hii?**

**RAIS MWINYI:** Kwanza, tumetoa elimu ya maana ya uchumi wa bluu, watu waelewe tukisema uchumi wa bahari au uchumi wa bluu ni kitu gani hasa. Si jambo jipya, ni utekelezaji tu kwa sababu utalii hapa Zanzibar kwa kiwango kikubwa ni uchumi wa bahari kwa sababu watalii walio wengi wanapenda utalii wa fukwe.

Uvuvi ni jambo ambalo lipo lakini tunataka lifanyike kisasa kwa maana watu wavue bahari kuu, kuwe na viwanda vya kusindika samaki, kuwe na uwezeshaji wa wavuvi wadogo na kuwapatia soko zuri.

Uchumi wa bluu ukiacha hayo masuala mawili ya utalii na uvuvi, pia kuna mafuta na gesi ambayo tumebahatika hapa Zanzibar kuwa nayo.

Tutaendeleza juhudi za kuhakikisha tunajenga miundombinu mizuri ya kuwawezesha wananchi wanufaike zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Hivi karibuni tulitia saini makubaliano ya awali ya ujenzi wa bandari kubwa kule Mangapwani. Eneo lile litakuwa na bandari za aina nyingi ambalo ndiyo kitovu cha uchumi wa Zanzibar baadaye.

Ni leo tu tumefanya makubaliano na kampuni nyingine ambayo yenyewe itajenga bandari ya uvuvi. Kutakuwa na sehemu ya viwanda vya kusindikika samaki na viwanda vya kuzalisha vifaa vya uvuvi.

Kwa hiyo, mwelekeo ni mzuri sana. Ni matumaini yangu wananchi wa Zanzibar watakuwa tayari kushiriki kikamilifu katika miundombinu hii inayojengwa ili hatimaye na wao wanufaike kimaisha.

*ITAENDELEA KESHO

**HABARI KITAIFA**

# Tanzania na Afrika Kusini zawasilisha ombi maalum AU

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Jamhuri ya Afrika Kusini zimewasilisha ombi maalumu kwa Umoja wa Afrika (AU) kuzitambua rasmi njia zilizotumika na wapigania uhuru kutoka Dar es Salaam kupitia nchi mbalimbali Kusini mwa Bara la Afrika hadi Namibia kuwa urithi wa kimataifa.

Ombi hilo liliwasilishwa na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, katika Mkutano wa 34 wa kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU unaofanyika kwa njia ya mtandao na kuungwa mkono na Serikali ya Tanzania kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, ambaye alimwakilisha Rais Dk. John Magufuli.

Tanzania pia imeomba AU kuitambua lugha ya Kiswahili kama lugha ya asili na ya ukombozi katika Bara la Afrika kwa kuwa ndiyo lugha iliyotumika kwa ajili ya mawasiliano na mafunzo kwa wapigania uhuru ikizingatiwa kuwa kauli mbiu ni sanaa, utamaduni na urithi.

"Tumeuomba Umoja wa Afrika kuitambua lugha ya Kiswahili kama lugha ya asili na ya ukombozi katika Bara la Afrika kwa kuwa ndiyo lugha iliyotumika kwa ajili ya mawasiliano na mafunzo kwa wapigania uhuru ikizingatiwa kuwa kauli mbiu ni sanaa, utamaduni na urithi," alisema Prof. Kabudi.

Akiufunga mkutano huo wa siku mbili, Mwenyekiti wa AU ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Felix Tshisekedi, alisisitiza kuwa umoja, mshikamano na amani katika Bara la Afrika ndiyo nyenzo pekee itakayoliwezesha bara hilo kuendelea kiuchumi ili kuendana na rasilimali ilizonazo.

Pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulijadili mambo mbalimbali ikiwamo uundaji wa kamati mpya ya uongozi wa AU kwa mwaka 2021, uzinduzi wa Kaulimbiu ya Umoja huo kwa mwaka 2021 inayohusu "Sanaa, Tamaduni na Urithi katika kufikia azma ya Afrika Tuitakayo."

Mengine yaliyojadiliwa ni taarifa ya Maendeleo ya Mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 barani Afrika, taarifa ya utekelezaji wa mabadiliko ya kitaasisi ya AU; na uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU.

Serikali ya Tanzania ilitumia fursa hiyo kueleza utayari wake kuendelea kushirikiana na AU na nchi Wanachama wa Umoja huo, katika kutekeleza jitihada zinazolenga kuiwezesha Afrika kujitegemea.



Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro, akisisitiza jambo kwa watumishi wa ofisi yake, jijini Dodoma, alipokutana nao kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakulima wa tumbaku wadai bil. 1.3/-

**Neema Sawaka,** KAHAMA

WAKULIMA wa tumbaku kutoka mikoa mbalimbali wanazidai kampuni nne za ununuzi wa zao hilo kiasi cha Sh. bilioni 1.3.

Madai hayo ni ya msimu wa mwaka 2019/2020 na kwamba kampuni hizo zilinunua kilo milioni nne za zao hilo kwa nchi nzima.

Hayo yalisemwa juzi mjini Kahama na Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku, Stanely Mnozy, na kusema kampuni hizo zilinunua kilo milioni nne nchi nzima kwenye maeneo yanayolima zao hilo yenye thamani ya Sh. bilioni 12.

Mnozya alisema wakulima waliouza katika kampuni hizo wanadai kiasi cha Sh. bilioni 1.3 na kwamba baada ya kushindwa kulipa wameamua kushikilia mali zao yakiwamo magari.

"Hata hivyo, mpaka sasa licha ya kampuni hizo kudaiwa kiasi hicho, zimeweza kulipa kiasi cha Sh. bilioni 10.8 kwa wakulima wa mikoa ya Katavi, Tabora, Shinyanga, Mbeya na Kigoma," alisema Mnozya.

Kampuni zinazodaiwa ni Magefa Growers Co. Ltd, Grand Tobacco Co. LTD, Pachtec Co. Ltd na Jespan Co.Ltd.

## Mfumuko wa bei waongezeka

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Januari 2021, umeongezeka kutoka asilimia 3.2 kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2020, hadi asilimia 3.5 kwa mwaka ulioishia mwezi Januari 2021.

Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na wadau imekamilisha zoezi la marejeo ya Fahirisi za bei za Taifa (FBT) kwa kutumia matokeo ya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya wa mwaka 2017/18.

Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii kutoka NBS, Ruth Minja, alibainisha hayo jana na kueleza kuwa mfumuko wa bei wa Taifa, umeongezeka hadi kufikia asilimia 3.5 kutokana na mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma.

## 'Corona haijaathiri upatikanaji mafuta'

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewatoa hofu Watanzania kwa kusema kuwa tishio la virusi vya ugonjwa wa corona halijaathiri upatikanaji wa mafuta nchini.

Aliyebainisha hayo ni Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ambaye alisema kuna ziada ya mafuta itakayotumia zaidi ya siku 30 na bado meli zinaendelea kupakua mafuta bandarini.

Dk. Kalemani alisema hayo jijini Dar es Salaam, wakati wa ziara ya kutembelea bandari ili kujiridhirisha kama kuna mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji yanayohitajika nchini, kwa kuwa nchi imeingia uchumi wa kati na miradi mingi mikubwa inaendelea kutekelezwa.

Alisema Tanzania imejipanga vizuri katika suala la upatikanaji wa mafuta, huku pia akiwatoa hofu Watanzania kuwa serikali inaendelea vizuri katika sekta hiyo kwani mpaka sasa, hakuna kiwango cha mafuta kilichopungua tangu kutangazwa kwa uwapo wa ugonjwa huo duniani.

Alisema kwa sasa, nchi ina mafuta mengi na ya kutosha, pia ziada ya lita milioni 209 kwa mafuta petroli, diseli lita milioni 121, mafuta ya taa lita 600,000 na mafuta ya ndege lita milioni 18, ambayo yatatosha kutumika kwa zaidi ya siku 30 zijazo na meli zinaendelea kupakua mafuta bandarini.

Alisema kuna meli iliyokuwa inapakua tani 38 za mafuta mwishoni mwa wiki.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuna mafuta ya kutosha siku zote ili miradi mikubwa ya kitaifa inayoendelea kutekelezwa kama ya reli ya kisasa (SGR), mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, miundombinu ya barabara, maji na mingine mingi isikwame kwa kukosa mafuta kutokana na ugonjwa huo.

"Ninawahakikishia Watanzania kwa niaba ya serikali kuwa mafuta yapo na yataendelea kuwapo, tumshukuru Rais wetu, Dk. John Magufuli kwa msimamo wake thabiti kwani anatuwezesha kufanya kazi usiku na mchana, hivyo hatutaweza kuathirika kwa yanayosemwa, tumekaa na wadau pamoja na wataalamu wetu tumeweka mpango na mikakati ya kuhakikisha mafuta yanapatikana muda wote," alisema Dk. Kalemani.

Nipashe

MWANGA WA JAMII

# Kuiongezea fedha TARURA matumaini kwa wananchi

**WIKI** iliyopita Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo, alitoa matumaini mapya kwa wabunge juu ya kupitiwa upya kwa kikokotoo cha bajeti ya ujenzi wa barabara zilizo chini ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Mapitio ya kikokotoo hicho yanafanywa na Bodi ya Mfuko wa Barabara, ili kuhakikisha kinakaa vizuri na mgao kwenda kwa usahihi na kumsaidia utendaji kazi.

Baadhi ya wabunge walieleza kero ya barabara za vijijini na mjini kwenye maeneo yao na kwamba licha ya fedha kutoa kidogo, lakini haigawanywi kwa usawa kwenye majimbo, jambo ambalo limesababisha maeneo mengine kukosa huduma bora za barabara.

Mbunge mmoja, alisema mtandao wa barabara za TARURA ni kilomita 130,000 na mtandao wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kilomita 40,000.

Lakini kwenye mgao wa fedha TARURA anapata asilimia 30 na TANROAD asilimia 70, jambo linalosababisha hali kuwa ngumu majimboni kwa kuwa barabara nyingi ziko katika hali mbaya.

Kilio cha wabunge ni cha msingi ni vizuri kuwa serikali imeipokea na kuahidi kukifanyia kazi, kwamba kiwango cha fedha kinachotolewa ni kidogo hakitoshelezi mahitaji.

Kwa ujumla barabara hizo ndizo zinaunganisha maeneo kwa kuharakisha maendeleo kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa kuwa kama kuna barabara za kiwango cha lami au changarawe maana yake zitapitika kwa mwaka mzima.

Kama barabara zitapitika maana yake wakulima watasafirisha bidhaa na kutafikia masoko kwa haraka narahisi zaidi, lakini wananchi watafikia huduma za kijamii kama za afya, elimu na maji kwa urahisi zaidi.

Lakini biashara kati ya mjini na vijijini itaimarika kwamba mfanyabiashara atakuwa na uhakika wa kununua bidhaa kutoka maduka makubwa ya mjini na kufikisha kijijini kwa ajili ya kuuza kwa urahisi zaidi.

Pia itakuwa ni rahisi watu kusafiri kutoka eneo moja hadi jingine kwa kipindi chote cha mwaka bila kujali kama ni masika au kiangazi, hivyo ni muhimu sana barabara hizo zikaangaliwa kwa umuhimu mkubwa ili kurahisisha shughuli za maendeleo.

Siku zote kukiwa na urahisi wa kwenda na kurudi vijijini yaani kuimarisha kwa mtandao wa barabara zote za mijini na vijijini kutasaidia kuimarisha shughuli za maendeleo ya pande zote.

Pia hakutakuwa na haja ya wananchi kukimbilia mjini kutafuta urahisi wa shughuli za kimaendeleo bali watazifanya mahali aliko na kuwa na uhakika wa kipato.

Ikiwa miundombinu itaimarishwa na umeme vijijini kufika kwenye vijiji mbalimbali maana yake shughuli za maendeleo zitakwenda haraka kwa kuwa barabara na umeme ni muhimu kuharakisha maendeleo ya watu.

Ni matarajio yetu marekebisho ya kikokotoo hicho yataleta tumaini jipya kwa wananchi wa mijini na vijijini na sasa tutaona mabadiliko na mgawanyo sawa wa fedha za ujenzi wa barabara hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Shule za umma nazo ni sehemu ya 'Speak English'

**KISWAHILI** ndicho kinachotumiwa kwa mawasiliano nchini na ndiyo lugha ya kufundishia shule za msingi za umma.

Lakini, mambo yanabadilika pale wanafunzi hao wanapohitimu elimu ya msingi na kuingia sekondari, lugha ya kufundishia si Kiswahili tena bali ni Kiingereza.

Kwenye shule za msingi za umma, Kiingereza ni somo, lakini sekondari ndiyo lugha ya kufundishia na mawasiliano, hivyo kwa kuwa huenda hawana msingi mzuri wa lugha wapo wanaokwama.

Mambo hayaishii hapo wanakuwa na kazi zaidi kwa vile wanapofika shuleni hukutana na vibao vimeandikwa 'Speak English', ni maelekezo ya kuzungumza Kiingereza.

Iwapo kwa miaka saba wamefundishwa kwa Kiswahili, huku Kiingereza likiwa ni somo, unatokea muujiza gani mara tu baada ya kuhitimu elimu ya msingi, wanakuwa tayari wajuzi na wazungumza lugha hiyo ya kigeni?

Kwa hali kama hii ni wazi suala la kuwataka wanafunzi wanaotoka shule za umma kuzungumza Kiingereza wanapokuwa katika mazingira ya shule litazamwe upya, kwa kuanza kuwajengea msingi bora wa lugha hiyo.

Hii inatokana na ukweli kwamba, lugha kuu za kufundishia ni hizo mbili, huku shule za msingi za umma kikiwa ni Kiswahili, lakini katika sekondari ni Kiingereza hapo inakuwa kama 'lugha gongana'.

Kumtaka mwanafunzi aliyehitimu serikali ya msingi katika shule umma azungumze Kiingereza anapokuwa shuleni ni mtihani asioweza kuujibu.

Tatizo hilo kwa wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi katika shule binafsi, halipo, kwa kuwa Kiingereza ndicho hufundishia, hivyo wanakwenda sekondari wakiwa na msingi wa lugha hiyo.

Ili kuondoa tabaka hilo, kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kuwawezesha wanafunzi kumudu lugha hiyo, badala kuwapo ambao wako mbele na wengine nyuma.

Badala ya Kiingereza kuendelea kubakia lugha ya kufundishia elimu ya sekondari na vyuoni, kishuke hadi shule za msingi, hasa za umma, ili wanafunzi wanaosoma huko waimudu.

Hatua hiyo, inaweza kuboresha ufahamu wa wanafunzi kwenye lugha hiyo, hivyo, wazazi, watunga sera na baadhi ya wataalamu wa masuala ya elimu walifanyie kazi.

Kimsingi kuna haja kusaidia kuboresha eneo hilo kuanzia shule za msingi ili wanafunzi wanapojiunga na sekondari, wawe na uwezo wa kutambua kile wanachojifunza kwa Kiingereza.

Wakati mwingine, inaweza kutafsiriwa kuwa mwanafunzi ana uwezo mdogo darasani na kumbe tatizo ni lugha tu, hivyo kuwapo kwa msingi bora wa Kiingereza tangu shule za awali ni jambo la muhimu.

Mwanafunzi anapokuwa na msingi huo tangu awali, anaweza kujiamini darasani na hawezi kubabaishwa na vibao vya 'Speak English', au 'English Speaking Area'.

Kama amejifunza Kiswahili muda wote, ghafla anaipoingia sekondari anaambiwa 'Speak English', hicho kimombo amejifunza lini?

Kwa hali kama hiyo, ni vyema mkazo wa kuwa na lugha ya kufundishia msingi na sekondari ikawa moja kuanzia awali, msingi, sekondari hadi vyuoni.

Hali ilivyo inaleta mkanganyiko kuona masomo yote kuanzia awali hadi msingi yanafundishwa kwa Kiswahili, lakini wanafunzi wanapojiunga na sekondari, Kiingereza kinakuwa lugha ya kufundisha, hali hiyo inawafanya waambulie patupu kwa sababu hawaielewi lugha inayotumika.

Ikiwezekana, si vibaya kuiga mfano kwa nchi za China, Urusi na nyingine ambazo zinafundisha masomo katika lugha zao, hali inayosaidia kuwafanya wanafunzi kuyaelewa kikamilifu.

Mazingira hayo yanaweza kusaidia hata Tanzania kuwa na wataalamu wa kiwango cha juu katika fani mbalimbali tofauti, kutokana na kujifunza kwa lugha yao na kuwa na uelewa mkubwa zaidi.

Si kuwa nakipinga Kiingereza, bali lengo ni kutaka wanafunzi wa shule za umma wasiachwe nyuma kwenye lugha hiyo ya kimataifa, lakini pia ninadhani si vyema kuwalazimisha kuiongea huku wakiwa hawaielewi.

# Wananchi waelimishwa kulinda shoroba

**Na Mwandishi wetu,** NAMTUMBO

WANANCHI wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma, wametakiwa kupunguza madhara yatokanayo na wanyamapori katika maeneo yaliyohifadhiwa na mapito ya wanyamapori (shoroba), ili kupunguza mzigo wa serikali kulipa fidia.

Wito huo ulitolewa na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Aden Nchimbi, wakati akizindua mpango wa utoaji elimu kwa wakazi hao namna ya kuwalinda wanyamapori kwenye maeneo waliyohifadhiwa.

Akizingumza kwenye uzinduzi wa utoaji elimu unaofanywa na Shirika lisilo la kiserikali la PAMS, linalojishughulisha na ufuatiliaji wa maeneo ya uhifadhi nchini, alisema elimu hiyo itasaidia binadamu kuwa salama dhidi ya wanyamapori.

Wananchi hao ni wanaoishi kwenye maeneo ya mapito ya wanyamapori ya Niassa ikiunganisha Pori la Akiba la Selous na Hifadhi ya Taifa Nyerere na nchi ya Msumbuji, na kwamba itasaidia wasiyaharibu ili wanyama wapite kwa urahisi bila usumbufu.

Meneja wa Miradi ya Uhifadhi wa PAMS, Maximillan Jenes, akielezea mpango huo wa utoaji elimu, alisema kuwa shirika limejipanga kwenda kutoa elimu hiyo kwenye vijiji hasa vilivyopo kwenye mapitio ya wanyama (shoroba).

Naye Rehema Kilindi alisema elimu hiyo itakuwa ni ukombozi katika pande zote mbili kwa binadamu na wanyama.

## Polisi Ruvuma yakamata silaha 160

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma limekamata silaha 160 zinazodaiwa kuwa ni haramu katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2020 pamoja na watuhumiwa 68.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Simon Maigwa, alilitaja tukio hilo ni la msimu wa mwaka mzima wa 2020 kufuatia misako kwa kushirikiana na kikosi dhidi ya ujangili pamoja na pori la akiba la Liparamba chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

Kamanda Maigwa aliziainisha silaha hizo ni magobore 149, Rifle 03 na Shortgun 8 na kwamba msako bado unaendelea wa kuzitafuta silaha nyingine pamoja na watu ambao wamekuwa wakimiliki silaha kinyume cha taratibu.

Keneth Sanga, Kamanda wa Kikosi dhidi ya Ujangili (KDU) mkoani humo, alisema silaha hizo zimekamatwa katika maeneo mbalimbali hasa yanayozunguka maeneo ya hifadhi ndani ya mkoa huo.

## Jamii yatakiwa kutoa damu kuokoa wengine

**Na Frank Monyo**

JAMII imetakiwa kujenga utamaduni wa kujitolea damu kwa wahitaji, ili kufikia mahitaji halisi ya damu ambayo ni kati ya chupa 500,000 mpaka 550,000 kwa mwaka.

Ushauri huo ulitolewa jijini Dar es Salaam na Ofisa Uhamasishaji kutoka Damu Salama, Fatuma Mjungu, wakati wa uchangiaji damu ulioratibiwa na Hospitali ya Aga Khan na kuhusisha vikundi mbalimbali vya wakimbia mbio za pole pole "Jogging" lililofanyika Chamazi.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati) na Kaimu Katibu Mkuu, Leonard Masanja (kulia), wakipata maelezo ya namna mafuta yanavyopimwa kutoka katika meli hadi kuwafikia walaji kupitia mita za kupimia mafuta (Flow Meter), wakati wa ziara ya waziri huyo, kujiridhirisha kama kuna mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji yanayohitajika nchini, iliyofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## PM kufungua maonyesho ya kuitambua mifuko wezeshi kiuchumi

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajia kufungua maonyesho ya nne ambayo ni kwa ajili ya kutambua mifuko inayowezesha wananchi kiuchumi katika kilimo.

Maonyesho hayo yatakayoanza leo yamekwisha nufaisha wakulima milioni 1.5 kupitia udhamini wa Taasisi ya PASS Trust.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa PASS Trust, Anna Shanalingigwa, alisema lengo la taasisi hiyo ni kuwezesha upatikanaji wa fedha kutoka taasisi za kifedha na kupatiwa wajasiriamali na wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo.

"Udhamini wetu kwa wafanyabiashara katika sekta hii unachangia pakubwa katika kuendeleza sekta ya kilimo, bila udhamini huu, wakulima kibiashara hawawezi kupata mikopo ya kuendeleza biashara zao.

Kwa hiyo PASS, inahakikisha inawasimamia wakulima hawa katika benki ili nao wapate mikopo," alisema Shanalingigwa.

Alisema taasisi hiyo, imeshirikiana na taasisi mbalimbali za kifedha nchini na kutoa dhamana ya mikopo kuanzia asilimia 20 hadi 80 kwa wanawake.

"Mfumo wetu unapendelea wanawake na vijana ambao wanapata dhamana ya hadi asilimia 80, ili kuwavutia vijana na wanawake katika kilimo biashara," alisema Shanalingigwa.

Kadhalika, aliongeza kwamba mnyororo wa kilimo, uvuvi na ufugaji, na kwamba wengne wanaohudumiwa ni pamoja na kampuni zinazojihusisha na sekta ya kilimo, vikundi vya wakulima, SACCOS, Vyama vya Ushirika na wakulima.

Pia alisema, mwaka jana taasisi hiyo, ilitunukiwa zawadi kwa kuunga mkono juhudi za serikali kutokomeza umasikini kwa kutengeneza fursa za ajira kupitia udhamini.

"Kufikia Septemba mwaka jana, udhamini wa PASS kwa makundi mbalimbali ulichangia upatikanaji wa ajira milioni 2.5.

Kipindi hiki, PASS inajivunia kudhamini takriban miradi 42,000 yenye thamani ya shillingi bilioni moja, wajasirimiali 1,593 wamenufaika na udhamini huu, asilimia 45 ya wanufaika wakiwa wanawake," alisema Shanalingigwa.

Alibainisha kuwa, taasisi hiyo imewezesha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ikiwamo vikundi vinayojihusisha na shughuli zinazoendana na kilimo katika mnyororo wa thamani.

"Kumiliki vifaa bila kuweka dhamana yoyote kama ilivyozoeleka kwenye taasisi mbalimbali za kifedha, kampuni hii imeshapata kibali cha muda kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ili kuanza kutoa huduma hii kwa wananchi

"Mwaka jana, sherehe za Nanenane, PASS ilinyakua tuzo ya taasisi bora nchini miongoni mwa taasisi zisizo za kiserikali kwa mchango wake katika kuinua sekta ya kilimo nchini."

# Wakazi Dar waijia juu TBA

**Na Maulid Mmbaga**

WAKAZI wanaoishi eneo la Wazo Tegeta Dar es Salaam, wamelalamikiwa kitendo cha kufukuzwa kwenye nyumba hizo na Wakala wa Nyumba (TBA) wakidai ni kinyume cha taratibu.

Aidha, wamedai kuwa madai ya kuwa wadaiwa sugu hayana msingi kwa kuwa wanalipa kodi stahiki, lakini baada ya mvutano walirudishiwa funguo na kuendelea kuishi wakati utaratibu wa kuanza kulipa viwango vipya vya kodi ukifanyika.

Mmoja wa waathirika, Grecy John, alisema amekaa kwenye nyumba hizo kwa zaidi ya miaka 20 na kodi waliyokuwa wanalipa ni Sh. 25,000, lakini kwa sasa wamepandishiwa kati ya Sh. 70,000 hadi 100,000 kiasi kisicholingana na thamani ya nyumba hizo.

Alisema TBA waliwafukuza kwenye nyumba hizo zilizopo ndani ya eneo la kiwanda cha saruji cha Twiga kwa madai wao ni wadaiwa sugu kwa zaidi ya miaka 10, jambo ambalo sio sahihi.

Kwa mujibu wa John, wana nyaraka zilizotolewa na Rais John Magufuli akiwa Waziri wa Ujenzi zikiagiza nyumba hizo ziuzwe baada ya mwekezaji kudai kwamba hazihitaji na zikakabidhiwa TBA kwa ajili ya kusimamia la uuzaji.

"Nyaraka hizo zinaeleza kwamba nyumba zinaporudi kwa TBA wasimamie uuzwaji wake na baada ya kupewa agizo hilo hakuna kilicho tekelezwa na badala yake walikaa kimya," alifafanua.

Aidha, aliongeza kuwa mwaka 2014, TBA ilifanya uhakiki wa wanaoishi ndani ya nyumba hizo na kuahidi kurudi kuzungumza nao, lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika, na waliletewa viwango vipya vya kodi ambavyo haviendani na agizo la kuuza nyumba hizo,

Aidha, alisema asilimia kubwa ya nyumba hizo ni mbovu na wataalamu walizifanyia tathmini na kuonyesha thamani yake ni sifuri hivyo wanashindwa kuelewa kwanini wanapandishiwa kodi.

Aidha, hakuna mwananchi aliyekataa kulipa kodi ila wanacho kilalamikia ni suala la TBA kuwapandishia tozo isiyoendana na uhalisia wa eneo husika hadi kufikia kuwafukuza kinyume na taratibu na kuwavika tuhuma za wadaiwa sugu pasipo kuwapa utaratibu uliotumika kupandisha kodi hizo.

# Mvua yaezua madarasa, nyumba za wakazi

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

MVUA kubwa iliyonyesha ikiwa imeambatana na upepo katika Kata ya Mbesa wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, imeezua madarasa 5 na ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi Liwawa na kusababisha wanafunzi wa shule hiyo kukosa sehemu ya kusomea.

Pamoja na tukio hilo, pia mvua hiyo iliyonyesha wastani wa saa moja kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 9.00 Februari 4, mwaka huu, pia iling'oa miti mikubwa ambayo iliangukia nyumba za wananchi pamoja na kuharibu kabisa majengo ya kutolea huduma za mapokezi kwa wagonjwa, njia za kupelekea wagonjwa wodini katika Hospitali ya Misioni ya Mbesa.

Taarifa zinaeleza kuwa sambamba na uharibifu wa miundombinu katika shule na hospitali hiyo, pia mvua hiyo iliezua zaidi ya nyumba 30 katika vijiji vya Mbesa ambako nyumba saba za Lijombo na kijiji cha Airpot ambacho nyumba 20 ziliezuliwa na nyingine kubomoka.

Diwani wa Kata ya Mbesa, Daniel Mlanda, alisema baada ya tukio hilo, familia zilizoathirika zinapata msaada wa makazi kwa majirani zao wakati taratibu za kuwasaidia kurejesha hali ya kawadi katika makazi yao zikiendelea kwa kusaidiwa na vijana wanaosomea ufundi kutoka Chuo cha Ufundi Nazereti kilichopo kijijini hapo, ikiwamo kuondoa miti zaidi ya 50 iliyo anguka maeneo mbalimbali.

Mtendaji wa Kata ya Mbesa, Abdalah Zuberi Mgwila, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo, na kwamba baada ya tukio hilo ofisi yake kwa kusaidiana na diwani walipeleka taarifa katika ofisi ya mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya, ili kuangalia uwezekano wa kuwasaidia haraka kufanya ukarabati wa madarasa yaliyoathiriwa na mvua hiyo katika Shule ya Mzingi Liwawa na kuwawezesha wanafunzi kuendelea na masomo.

Mgwila alisema tayari kikao cha maendeleo ya kata WADC na mkutano wa wananchi imepitisha mapendekezo ya kuwahamishia wanafunzi wa darasa na nne na la saba katika shule jirani za vijiji vya Airport na Mbesa ili kuwawezesha kuendelea na masomo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Gasper Balyomi, alisema amekwisha peleka wataalamu wake kutoka idara ya ujenzi kwa ajili ya kwenda kufanya tathmini ili kutengeneza bajeti ya kuanza ukarabati wa majengo hayo haraka.



Wakazi wa Goba Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana, wakiangalia Mto Mbezi unavyozidi kubomoa makazi yako kutokana na kutokuwa na kingo za kuzuia maji. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# LHRC yazindua mpango wa haki za binadamu

**Na Elizabeth Zaya**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani Machi 3, mwaka huu, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimezindua mpango maalum unaojulikana kama 'Haki Marathon' wenye lengo la kukuza uelewa juu ya umuhimu wa kulinda na kuheshimu haki za binadamu nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Anna Henga, alisema wanafanya hivyo kwa ajili ya kuongeza uwajibikaji na uwazi katika kulinda na kutetea haki hizo za binadamu.

Pia alisema ni kukemea na kukomesha vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ambavyo bado vinaendelea kufanyika nchini.

"Ili kukuza umoja na ushirikiano baina ya wadau wa haki, LHRC tunatarajia kuwaleta pamoja wadau kutoka sekta binafsi, serikali, asasi za kiraia, pamoja na vilabu vya haki za binadamu vilivyoko hapa nchini," alisema.

"Ni imani yetu kuwa Haki Marathoni itaikumbusha jamii kuhusu umuhimu wa kushirikiana kwa pamoja katika kutafuta jamii yenye haki na usawa."

Henga alisema ripoti iliyotolea na LHRC mwaka 2019, inaonyesha ukatili dhidi ya wanawake umeongezeka, na kwamba kuna haja suala hilo likaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

"Ripoti hii ilibainisha kuwa kwa mwaka 2019 kuanzia Januari hadi Juni matukio 3,709 ya ubakaji wa wanawake na watoto yaliripotiwa katika vituo vya polisi nchini," alisema Henga.

"Hivyo tunaamini programu hii itasaidia kukuza uelewa kuhusu madhara ya unyanyasaji wa kijinsia pamoja na umuhimu wa kulinda na kuheshimu haki za binadamu. Ni imani yangu kwamba mpaka kufikia mwaka 2030 nchi yetu itafikia malengo endelevu tuliyojipangia ikiwamo la kukomesha umaskini na kufikia jamii yenye usawa."

## HABARI KITAIFA

# Wakamatwa wakidaiwa kuingia nchini kinyemela

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

IDARA yaUhamiaji Mkoa wa Kigoma imewakamata raia wa kigeni 52 wanaodaiwa kutoka Burundi na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) walioingia nchini bila vibali. Wanadaiwa kuwamo wakimbizi 12 waliotoroka katika Kambi ya Nyarugusu iliyoko Wilaya ya Kasulu.

Kaimu Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Kigoma, Augustino Matheo, alisema msako uliofanyika Februari 5 na 6 katika maeneo mbalimbali mkoani humo ulifanikisha kukamata raia 43 kutoka Burundi kati yao wakiwamo wakimbizi 3 na raia kutoka DRC 9 ambao ni wakimbizi kutoka kambi ya Nyarugusu.

“Katika msako huo kuna raia wa wanne kutoka Burundi, tumewakamata wakiwa njiani kuelekea Mwanza wakiwa na hati za kusafiria zilizoghushiwa mihuri ya Idara ya Uhamiaji,” alisema.

Matheo alisema kuna Watanzania watatu wamekamatwa katika msako huo kutokana na kuwapa hifadhi watuhumiwa hao, na kwamba wote watafikishwa mahakamani wakati wowote.

Hivyo kuwataka wananchi mkoani Kigoma kuacha kuwaajiri kwenye shughuli za kujipatia kipato bila kufuata taratibu za uhamiaji, kwani sheria ya uhamiaji inatoa adhabu kwao pia.

**Katika msako huo kuna raia wa wanne kutoka Burundi, tumewakamata wakiwa njiani kuelekea Mwanza wakiwa na hati za kusafiria zilizoghushiwa mihuri ya Idara ya Uhamiaji,” alisema.**

# Waonywa kuingiza bidhaa bila kulipa kodi

**Na Gideon Mwakanosya, NYASA**

MKUU wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba, amewataka wajasiriamali na wafanyabiashara wa Wilaya ya Nyasa kufanya biashara halali, na kulipa kodi halali.

Ameyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akizungumza na wafanyabiashara wa Wilaya ya Nyasa katika kikao cha kujadili mambo mbalimbali na masuala ya maendeleo.

Chilumba alifafanua kuwa, wafanyabiashara na wajasiriamali wa Wilaya ya Nyasa wamekuwa wakivunja sheria kwa kukaidi kulipa kodi na kuingiza bidhaa mbalimbali, kutoka nje ya nchi hususani Msumbiji na Malawi kwa njia za panya, ili kukwepa kulipa kodi halali ya serikali, hivyo kuikosesha serikali mapato, ambayo yangeweza kujenga miundombinu ya nchi.

Aliongeza kuwa aliamua kuitisha kikao hicho kutoa elimu kwa wafanyabiashara hao, ili kuelewa umuhimu wa kulipa kodi za serikali, na kuwaagiza na kuacha mara moja tabia ya kuingiza kiholela kwa njia za magendo bidhaa mbalimbali kama mafuta ya kupikia, yanayotoka Msumbiji na sukari inayotoka Malawi.

Kwa upande wao wafanyabiashara hao waliiomba serikali kupunguza ushuru na tozo hasa katika bidhaa za nje kwa kuwa ndio sababu zinazowafanya wakwepe kodi kutokana na kutopata faida.

Ofisa Biashara wa Wilaya ya Nyasa, Zaitun Hamza, aliwataka wafanyabiashara hao kufahamu kuwa viwango vya kodi wanazotozwa, ni kwa mujibu wa sheria ya kodi, hivyo hakuna anayeweza kupunguza viwango hivyo.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, akionyesha silaha 160 za aina mbalimbali zilizokamatwa na jeshi hilo, kufuatia misako iliyofanywa katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHAVITA yanolewa kuhusu ufugaji nyuki

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WANACHAMA 30 wa Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Kutosikia (CHAVITA) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamepatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ili kujikwamua kiuchumi na kuacha kuomba mitaani.

Akifungua mafunzo hayo, kaimu Meneja wa TFS, Ester Josephati, alisema watawezesha wanachama hao ili kufikia malengo yao waliojiwekea baada ya kupatiwa mafunzo.

Alisema kabla ya kupatiwa mafunzo hayo waliandika barua kuomba kupewa mafunzo ya ufugaji wa nyuki, utengenezaji wa mkaa mbadala ili kuendelea kujikwamua kiuchumi.

Awali akitoa mafunzo hayo Ofisa ufugaji nyuki kutoka TFS, Martha Machibya, alisema wamekuwa wakitoa elimu hiyo kwa vikundi mbalimbali vya ujasiriamali.

Aidha, alisema mwaka wa fedha 2014/2015, TFS ilitoa mizinga ya ufugaji nyuki 200 kwa vikundi vya ujasilimali na mwaka 2015/2016 ilisitisha utoaji wa mizinga hiyo.

# Waeleza TASAF ilivyowanufaisha

**Na Richard Makore, SENGEREMA**

BAADHI ya wanufaika wa mpango wa kusaidia kaya maskini unaoratibiwa na serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), mkoani Mwanza wamempongeza Rais John Magufuli kwa kuendelea kuwajali na kusaidia.

Wanufaika hao ambao walianza kusaidiwa fedha za ruzuku mwaka 2015, walisema tangu wakati huo maisha yao yamebadilika. Walisema kila kaya inapata wastani wa kati ya Sh. 32,000 hadi 80,000 kwa mwezi kiasi ambacho kimewasaidia kujikwamua kiuchumi.

Tabu Kahama, mkazi wa mjini Sengerema mkoani Mwanza, alisema ruzuku hiyo imemwezesha kusomesha watoto wake, kununua mbuzi pamoja na kupata bima ya afya.

Marysiana Nyasenga aliwaambia maofisa wa TASAF waliomtembelea nyumbani kwake kuwa ruzuku anayoipata imemwezesha kulima na hivyo kupata mazao ambayo aliyauza na kujenga nyumba ya bati.

Marysiana Chigula alisema wamebahatika kupata watoto saba ambao wote wamemudu kuwasomesha kupitia fedha wanazopewa kila mwezi.

Mratibu wa TASAF, Wilaya ya Sengerema, alisema kati ya mwaka 2015 hadi 2021 jumla ya wanufaika 5587, walipewa ruzuku ya kusaidia kaya maskini.

Alisema katika kipindi hicho, wametoa ruzuku ya Sh. bilioni 12.4 kwa wanufaika hao na kwamba fedha hizo zimesaidia kuboresha maisha yao.

Aliongeza kwamba baada ya kutoa fedha hizo, wanakwenda kuwatembelea nyumbani kwao na kuwapa ushauri ili waweze kutumia ruzuku hiyo vizuri na kuwanufaisha.

# Utekelezaji maamuzi ya mawaziri migogoro ya ardhi hifadhi kuanza

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema utekelezaji wa maamuzi ya Kamati ya Mawaziri iliyoundwa kupitia maeneo yenye migogoro ya wananchi na hifadhi za taifa utaanza baada ya kumalizika kwa mkutano huu wa Bunge.

Aidha, imeahidi kwenda na wataalamu kuonesha wananchi mipaka katika Hifadhi ya Taifa Kitulo.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akijibu maswali ya wabunge kuhusu migogoro ya wananchi na hifadhi za taifa.

Katika swali la Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga, aliyetaka kujua ni lini serikali itarudia zoezi la kuweka alama za mipaka kwa kuwashirikisha wananchi ili kumaliza mgogoro uliopo wa mipaka kati ya Hifadhi ya Taifa Kitulo (TANAPA) na wananchi wa Vijiji vya Misiwa, Makwalanga, Igofi na Nkondo.

Mbunge huyo alisema uwekaji mipaka huo umesababisha baadhi ya wananchi wake kuwekwa rumande na kumwomba Naibu Wizara huyo kwenda na wataalamu kupitia upya mipaka na kutoa suluhisho.

Akijibu swali la Sanga, Masanja alisema kamati hiyo ilishafanya maamuzi ikapitia baadhi ya maeneo yenye migogoro na maamuzi hayo yataanza kutekelezwa baada ya Bunge hilo na vijiji 920 vitafaidika.

Awali, alisema mwaka 2016, serikali ilishaweka alama za mipaka za kati kwenye maeneo ya Hifadhi ya Taifa Kitulo inayopakana na vijiji vya Misiwa, Mwakalanga, Igofi na mwaka 2018 katika Kijiji cha Nkondo.

"Zoezi hili la uwekaji wa alama lilishirikisha Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Makete, Waheshimiwa madiwani, Serikali za Vijiji, wananchi kwa ngazi ya vijiji, pamoja na wataalamu wa ardhi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Makete, elimu iliyotolewa kwa wananchi kuhusu zoezi la uwekaji alama za mipaka kwenye vijiji hivi kabla ya uwekaji wa alama za mipaka hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema baada ya utoaji wa elimu, wananchi walichagua wawakilishi watano katika kila kijiji ili kujiunga na timu ya watumishi kutoka hifadhini na wataalamu wa ardhi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Makete, ili kufanya utambuzi wa eneo la mipaka na kuweka alama hiyo kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na.279 ya Mwaka 2005 ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa Kitulo.

"Naomba kutoa taarifa kwamba maeneo hayo tajwa yalikwisha wekewa alama za mipaka na zoezi hilo liliwashirikisha wananchi kikamilifu, lengo kuu la zoezi hilo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa mipaka inaonekana bayana, na pia shughuli za kibinadamu hazifanyiki ndani ya eneo la hifadhi," alisema.

Alisema serikali inaamini mgogoro wa mipaka kati ya Hifadhi ya Taifa Kitulo na vijiji vilivyotajwa ulishapatiwa suluhu kwa kuzingatia Tangazo la Serikali na kuomba wananchi ushirikiano wao ili kuhakikisha kuwa wanashiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi.

Katika swali la Mbunge wa Babati Vijijini (CCM), Sillo Baran, alihoji lini serikali itamaliza migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi ya Taifa Tarangire na vijiji vya Gijedabung, Ayamango, Gedamar na Mwada katika Jimbo la Babati Vijijini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema mgogoro wa mpaka baina ya Hifadhi ya Taifa Tarangire na vijiji vya Wilaya ya Babati umemalizika huku kaya 256 zililipwa fidia ya Sh. milioni 175.05 kati ya mwaka 2009 na 2011.

Pia, swali la Mbunge wa Namtumbo (CCM), Vita Kawawa, alisema kumekuwa na ongezeko la wanyamapori katika Hifadhi ya Mbuga ya Selous na sasa tembo na nyati wanavamia mashamba pamoja na makazi ya wanavijiji na kuleta taharuki.

"Je, serikali inaweza kuwarudisha wanyama hao porini mbali zaidi na wananchi?" Alihoji.

Naibu Waziri Masanja akijibu swali hilo, alisema wizara imeandaa na inatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Aidha, alisema wizara inaendelea kukamilisha utaratibu wa kuweka alama katika shoroba na mapito ya wanyamapori ili kuimarisha uhifadhi wake na kuendelea kufanya utafiti na kueneza matumizi ya mbinu mbadala za kujikinga na wanyamapori waharibifu hasa tembo.



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na wanafunzi kutoka Umoja wa Wanafunzi Vyuo Vikuu nchini, wa mikoa mbalimbali nje ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma, jana. **PICHA: BUNGE**

# Mbunge ataka tume kuchunguza unyanyasaji wa askari Magereza

MBUNGE wa Kwela (CCM), Deusi Sangu, ameomba kuundwa kwa tume ya kuchunguza unyanyasaji unaofanywa na askari wa Jeshi la Magereza Mollo Sumbawanga kuhusu tamko la Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, la kutoa shamba lenye ukubwa wa ekari 495 kwa wananchi wa vijiji vya Msanda Muungano, Songambele na Sikaungu.

Akiuliza maswali ya nyongeza bungeni jana, Sangu alisema Jeshi hilo linasema haliwezi kufanyia kazi matamko ya wanasiasa hadi lipate barua kutoka wizarani.

"Tamko hili limesababisha askari Magereza sasa kuingia mgogoro na wananchi kuwapiga na juzi mama mmoja amepigwa na kugalagazwa kwenye matope, je, wizara ipo tayari kuunda tume kuchunguza manyanyaso haya na itakapobainika hatua za kisheria zichukuliwe ili iwe fundisho kwa wengine," alisema.

Aliomba serikali kutimiza ahadi ya kukabidhi shamba lililokuwa limechukuliwa na Jeshi la Magereza Mollo Sumbawanga kwa wananchi na ni ahadi ya Waziri wa Mambo ya Ndani wa wakati huo mbele ya Rais alipofanya ziara Mkoa wa Rukwa ambapo aliahidi kuwakabidhi wananchi.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamza Khamis Khamis, akijibu swali hilo, alisema wizara itachunguza na ikibaini kuna watu wanahusika hatua kali zitachukuliwa dhidi yao kupitia Jeshi la Magereza.

Awali, alisema Jeshi hilo na wananchi wa vijiji hivyo walikuwa na mgogoro ambao ulimalizwa mwaka 2019 kwa serikali kutoa eneo la ekari 1,800 kwa lengo la kumaliza mgogoro kama walivyohitaji, huku akisema hitaji la ekari 495 ni dai jipya ambalo wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza na Ofisi ya Mkoa wa Rukwa litaendelea kulifanyia kazi.

## Muswada wa sheria usalama barabarani mbioni kukamilika

BUNGE limeelezwa kuwa muswada wa sheria ya usalama barabarani ya mwaka 1973 upo mbioni kuletwa bungeni ili kufanyiwa marekebisho.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamza Khamis Khamis, aliyasema hayo akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba, alisema lipo tatizo la msingi la ajali za barabarani kwa bodaboda na vyombo vingine vya barabarani.

"Tatizo hili linasababishwa na baadhi ya askari wa kitengo cha usalama barabarani kugeuza kitengo hicho kama chanzo cha mapato ambapo watu wanakwepa matrafiki na kukimbia kwa sababu mtu akikamatwa hakuna faini kuna onyo," alisema.

Alihoji: "Bodaboda siku hizi wanakimbizana na matrafiki wanakamatwa, hii inasababishwa na uzee wa sheria hii ya mwaka 1973, je, ni lini serikali italeta mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani bungeni ili tufungue mjadala wa namna gani tutaibiresha kupunguza ajali za barabarani."

Naibu Waziri huyo akitoa majibu ya swali hilo, alisema muswada huo upo njiani na utaletwa kujadiliwa ili kufanya marekebisho ambayo yanashauriwa na wadau.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jackline Kainja, alitaka kujua mpango wa serikali wa kutoa elimu ya sheria ya usalama barabarani kwa madereva wa bodaboda ili waendeshe kwa kutumia sheria hizo na kuepuka kusababisha ajali.

Alisema licha ya kupunguza ajali mwaka 2019 zilikuwa 567, lakini mwaka 2020 zilikuwa 240.

"Jeshi la Polisi lina mpango gani katika kuhakikisha ajali hizo zinapunguza zaidi kwani wahanga ni vijana," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alifafanua kuwa Jeshi la Polisi kwa kupitia kikosi cha usalama barabarani limekuwa likitoa elimu kuhusu sheria ya usalama barabarani kwa madereva wa bodaboda na watumiaji wengine wa barabara na vyombo vya moto kwa kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani yaani The Road Traffic Act No.68/19733, RE.2002 na GN 144/2010.

Alibainisha kuwa elimu hiyo hutolewa kwa kupitia maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama barabarani, televisheni, radio, magazeti, vipeperushi, maadhimisho ya sabasaba na nenane, matamasha mashuleni na kwenye vijiwe na kwenye maskani ya bodaboda.

Aidha, alisema katika kipindi cha kuanzia Januari mpaka Desemba, 2020 jumla ya vipindi 399 vya elimu ya usalama barabarani vimerushwa hewani na kuoneshwa mubashara kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na vituo 89 vya radio na televisheni, na pia elimu imetolewa kwa madereva wa bodaboda 638,275 na kwenye vijiwe vya bodaboda 7760 nchi nzima.

"Wizara inashukuru wadau mbalimbali katika kutoa elimu hiyo ambao ni TRA, PUMA, AAT, APEC, Future World Training Colledge na Amend, lengo ni kujenga ufahamu wa sheria na kuepusha ajali kwa madereva wa bodaboda na watumiaji wengine wa barabara," alisema.

Nipashe
TESA
Jumanne Februari 9, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 13

Ndivyo Magereza inavyoliokoa taifa na mbegu 'zinazoogopwa'



Ukurasa 14

Mkoa ulivyounda mabaraza vijiji, kukomesha ubakaji, ndoa utotoni

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

### KHE INASHAGAZA!...

# Madawati yabaki tupu darasani, kisa mabinti wapewa ujauzito

WANAFUNZI zaidi ya 20 waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu wilayani Serengeti katika mkoa wa Mara, wamebainika kuwa ni wajawazito hivyo hawakuanza masomo ya sekondari Januari 2021, hali inayopunguza wasichana madarasani na kuwarudisha nyuma kitaaluma.

Ni kwa mujibu wa maelezo ya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu, anayoyatoa kwa wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wilaya, akisema tatizo hilo ni kubwa na linaathiri maendeleo ya elimu kwa wasichana.

"Tayari watuhumiwa wanne wameshakamatwa kuhusika na matukio hayo ambayo ni kikwazo kwa maendeleo ya elimu ya mabinti, inatakiwa kuanzia sasa kila mmoja ayapige vita mambo haya," anasema Babu na kuongeza kuwa hata wakati wa likizo ya corona, zaidi wanafunzi 28 wa sekondari na msingi, walipata mimba.

"Lakini bahati mbaya baadhi ya viongozi wa maeneo yanayoripotiwa kuwapo kwa mimba hawachukui hatua wala kushughulikia tatizo hilo kwa kukamata wahusika, hali inayochangia kuendelea," anasema.

Si kwamba ni tatizo la Serengeti pekee bali pia ni karibu nchi nzima, kwa kuwa kuna mifano mingi, ukiwamo wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 184 mkoani Pwani waliopata mimba na kuacha shule mwaka 2019.

Hayo yanabainishwa katika kikao cha wadau wa elimu kujadili hali ya elimu kimkoa, huku mkuu wa mkoa wa Pwani Evarist Ndikilo, akisema, wanafunzi 144 walikuwa ni wa sekondari na 40 wanatoka shule za msingi.



Wanafunzi wa kike kama hawa wanatakiwa kulindwa dhidi ya mimba, ili watimize ndoto zao katika elimu. **PICHA: MTANDAO**

Wilaya ya Serengeti inatajwa kuwa ni miongoni mwa zile ambazo zimefanya juhudi katika ujenzi wa madarasa yanayokidhi mahitaji na kuwa na ziada mkoani Mara na itajwa kuwa ni mfano wa kuigwa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Carolina Mthapula ndiye anayesema hayo wakati akitangaza matokeo ya wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza mwaka 2021 na kuongeza:" Niwaombe wadau wenye uwezo kutuchangia kupitia halmashauri zetu ili kukamilisha kazi hii ya ujenzi wa madarasa ili watoto wetu waanze kusoma mapema iwezekanavyo."

Anasema, kati ya wanafunzi 51,822 waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka jana, 40,426 wamefaulu, ambao ni sawa na asilimia 77.98, na kwamba kati ya wote waliofaulu mtihani huo, wavulana ni 20,950 wakati wasichana ni 19,476, na kufafanua kwamba, kuna wanafunzi 11,396 ambao walifanya mtihani huo, lakini hawakufanikiwa kufaulu.

Kwa upande wake Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mara, Freedence Serapion, anasema wanafunzi hao walikuwa ni 62,596, lakini waliosajiliwa kufanya mtihani wa mwisho ni 51,882, wengine 1,361 hawakufanya mitihani kutokana na sababu mbalimbali na kuongeza kuwa ufaulu wa wanafunzi kwa ngazi ya mkoa umepanda kwa asilimia 8.24 huku Serengeti ikiongoza kwa kufanya vizuri zaidi kuliko wilaya nyingine za mkoa huo katika matokeo ya mtihani huo.

Serengeti inatajwa kufanya vizuri, lakini inaharibiwa na tatizo la mimba ambalo linakwamisha maendeleo ya elimu kwa wanafunzi wa kike, hivyo juhudi za kulimaliza zinatakiwa kufanywa na wadau wote na kuwataka wazazi, walezi na viongozi wa maeneo husika kuwa mstari wa mbele kukemea ukatili huo unaofanywa na mafataki ili usawa wa kijinsia katika elimu uonekane.

**KIKWAZO KINGINE**

Hadi Desemba mwaka jana, watoto wa kike 55 wakiwamo wanafunzi, walikuwa wamehifadhiwa nyumba salama ya mjini Mugumu ya Hope for Girls baada ya kukwepa ukeketaji unaofanywa nyumbani kwao, anasema Mkurugenzi wa Hope for Girls, Rhobi Samwelly na kuongeza kuwa tayari wamesharudishwa kwa wazazi wao ili waendelee na masomo, baada ya kuhakikishiwa kuwa hawatakeketwa.

"Hope for Girls kwa kushirikiana na wadau wa utetezi wa mtoto wa kike wakiwamo Dawati la Jinsia na Ustawi wa Jamii tumewarudisha kwa wazazi wao kwa masharti," anasema Rhobi na kuyataja kuwa ni pamoja na wazazi kujaza fomu maalum wakikiri kutojihusisha tena na vitendo hivyo kwa watoto wao na kwamba watoto wanaokataa kurudi kwao hubaki kituoni hapo.

"Wanaohofia usalama wao, hubaki nyumbani salama na kutafutiwa uhamisho wa kuwawezesha kusoma shule za mjini, kwa kuwa hatutaki kuwalazimisha kurudi kwao bali wanatakiwa kuondoka kwa hiari yao," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema kama watetezi wa haki na ulinzi wa mtoto wa kike, wanalaani ukeketaji, na kwamba wazazi na walezi wanaoendekeza vitendo hivyo ndoa za utotoni, wanakwamisha mtoto wa kike kupata elimu.

**KUFIKIA LENGO NAMBA 4**

Rhobi anasema kabla ya kufikia lengo endelevu namba nne ambalo ni elimu bora na ya usawa kwa

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

MARTHA MGANGA (2)

# Baada ya kunusurika kifo, ageuka ngao wenye ualbino

SISTA Martha Mganga, ni mwanamama ambaye baada ya kunusurika kifo, alitoa ahadi kwa Mungu kuwa atawahudumia watu wanaoishi na ualbino, kuwafariji na kuwapa msaada wanaohitaji kadri atakavyojaliwa.

Anaweka nadhiri hiyo kwa sababu alifikia hatua ya kukatisha maisha yake, kwa kujirusha ndani ya Mto Nduruma ulioko Arusha mjini wakati ukiwa umejaa na kufurika, msimu wa masika ili afe, asiendelee kudhalilishwa, kukataliwa na kunyanyapaliwa kila anapoonekana, kisa, amezaliwa na ualbino.

Baada ya kujitosa mtoni usiku wa manane, alinusurika kwa vile mawimbi yalimrusha nchi kavu na kuokolewa akiwa salama asubuhi, na huo ukawa mwanzo wa maisha mapya katika huduma, akianzisha Shirika la Peace Makers for Albinism and Community linaloendelea kutetea ustawi wa wenye ualbino popote nchini, likiwa na makao yake jijini Arusha.

Wiki mbili zilizopita tuliandika simulizi lake na leo tunalikamilisha. Sista Martha, ni mwinjilisti wa Anglikana na pia ni mwalimu ambaye baada ya kuteswa na kupewa majina mengi kisa kuzaliwa na ualbino, anatafuta majibu ya maswali yanayowakabili na kuwasaidia wanaoishi na ualbino.

Martha anasema, kiini na changamoto za wenye ualbino ni jamii kutofahamu ukweli kuwa kuishi na ualbino ni hali ya maumbile na kama walivyo watu wengine, wenye ualbino hawana tofauti, ila wana upungufu wa rangi ya asili ya ngozi.



Martha pamoja na watoto anaowalea katika makazi yao yaliyoko jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**JUHUDI KITAIFA**

Anasema, katika kusaidia kupunguza unyanyapaa na kuifanya jamii kukubali kuwa si laana wala balaa kuzaliwa na ualbino anahamasisha na kutoa elimu kwa jamii kukubali na kufahamu ukweli kuhusu 'albinism' na kwamba ili kuwe na mafanikio ni vyema wakunga wa jadi na wa mahospitalini wakafahamu kuhusu hali hiyo na kuwasaidia wazazi wanaojifungua ili kuwakubali na kuwatunza watoto wanaowapata.

Martha anapozungumza na Nipashe anasema, muuguzi au mkunga ndiye wa kwanza kumwona mtoto mama anapojifungua, hivyo ni vyema wakaelimishwa kuhusu hali ya ualbino ili wawashauri wazazi hao kuwa hata kama baba na mama hawana ualbino wanaweza kupata mtoto mwenye ualbino kwa sababu wana nasaba zake.

"Wazazi wangu walikuwa weusi lakini tumezaliwa watoto watatu wenye ualbino. Ni kwa sababu wazazi wetu wote walikuwa na vinasaba vya ualbino. Ni lazima wote wawili wawe navyo. Ndiyo maana wakunga na wauguzi wakifahamu itakuwa rahisi kuwaelimisha wazazi kujikubali na kumkubali mtoto."

Anasema, amefanya kazi ya kutoa elimu kwa wauguzi, wataalamu wa ngozi, madaktari wazazi na wauguzi katika hospitali kadhaa ikiwamo Seliani mkoani Arusha, na kwamba, amefikisha juhudi kwa wadau kama hao sehemu nyingi na katika hospitali za kanda ya ziwa.

Martha anasema, ameelimisha madakatari, wataalamu wa ngozi wakiwamo wanaohudumu katika vituo vya afya vya kata na hospitali za wilaya vya kanda hiyo na kuwafikia wataalamu hao katika mikoa ya Mara kama hospitali za Musoma, Bunda, Buhemba, Musoma Vijijini.

Pia amewafikia wataalamu hao katika mikoa ya Shinyanga, Singida, Dodoma na Kigoma, na kwamba, juhudi zinaendelea hasa maeneo ambayo kuna shida ya kuwakataa na kuna unyanyapaa wa wenye ualbino.

Katika juhudi hizo anashirikiana na wadau wengi wakiwamo wakunga wa jadi na viongozi wa dini kuelimisha jamii na kusambaza ujumbe wa kuwakubali na kuwasaidia wenye ualbino.

Anakumbusha kuwa, wanafanya hivyo ili kuwawezesha wazazi na jamii kujikubali, kumkubali na kumlea mtoto kwa upendo bila ubaguzi na unyanyapaa na kuwaelezea kuhusu changamoto wanazokumbana nazo na kuwatia moyo na kuwahamasisha kusonga mbele kwani wanaweza.

Martha kupitia Peace Maker for Albinism and Community, anayesaidia watoto wenye ualbino zaidi ya 166, ambao ni wanafunzi shule za msingi, sekondari, vyuoni, wakiwamo wanaoishi bweni, anasema, kushirikiana na madaktari na wakunga walio karibu wakati wa uzazi ni njia muhimu ya kufanikisha kuwakubali watoto wanaozaliwa na ualbino.

**KUWALEA KIAFYA**

Katika mahojiano hayo, anawashauri wanaolea watoto wenye mahitaji maalumu kuwapenda na kuwahudumia au kuwasiliana na taasisi zinazosaidia ustawi wao ili kufanikisha juhudi za kuwawezesha kukua na kufurahia maisha yao.

Anakumbusha wakati wa jua kali kuwashauri wasikae juani, wavae mavazi marefu ya kufunika ngozi, kofia na miwani kuficha kichwa na uso na kuwasaidia kupata tiba kwa kuwa ngozi yao inapopata vidonda inachukua muda mrefu kupona.

Anawashauri wazazi na walezi kuwapa watoto vyakula vinavyoimarisha kinga ya mwili, bila kusahau vitamin, maji mengi, matunda na mboga pamoja na karoti kwa wingi ili kuimarisha afya ya ngozi na macho.

Anasema, katika maelezo ya wenye ualbino, kila swali linalowagusa lipatiwe majibu, mfano kama wana uoni hafifu wapewe vifaa saidizi kama miwani, vikuza herufi (telescope na monocular) kukaa mbele darasani pamoja na kusoma machapisho yenye picha kubwa na maandishi makubwa.

Martha anashauri kuwa kuwatia moyo wanaoishi na ualbino kwa kuwapa mifano ya watu wanaoishi na ulabino waliofanikiwa, pamoja na kuwajengea mazingira ya kusonga mbele na kuondoa hofu ni masuala muhimu wakati wa kumsaidia na kumlea mtoto mwenye ualbino.

# Madawati yabaki tupu darasani, kisa mabinti wapewa ujauzito

INATOKA UK.11

wote, linatangulia namba 3 linalolenga afya na ustawi bora kwa jamii, ambapo kwa namna moja ama nyingine, yanasaidia kulifikia lengo namba 5 na kwamba lengo hilo namba 5, linasisitiza usawa wa kijinsia, hatua ambayo inaweza kusaidia kulifikia lengo namba 11 ambalo linalolenga kuwa na jamii endelevu ifikapo mwaka 2030.

Anasema ili watoto wote wawe na mwanzo bora na ustawi maishani, ni muhimu lengo hilo namba 4 litekelezwe vyema kwa kuhakikisha kila mmoja wao apate elimu huku akiepushwa na mazingira yanayoweza kumkwamisha.

"Hivyo kama jamii inataka kushughulikia janga la elimu na wanafunzi wa kike ili waweze kufikia kiwango cha kusoma na kuandika sambamba na ufahamu wa kutosha, ni muhimu kuwekeza kwa watoto kwao.Lakini ili kufanikiwa na kupata matunda ya malengo hayo na mengine, ni vyema kujali haki za watoto ili kupata kizazi bora cha siku za usoni ingawa safari hiyo bado ni ndefu." Anasema Rhobi.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# 'BYE' HOFU GMO

# Ndivyo Magereza inavyoliokoa taifa na mbegu 'zinazoogopwa'



Mbegu zipo za aina mbalimbali, lakini kinachohitajika ni uhakiki wa ubora na usalama ili kulinda afya za walaji. **PICHA: MTANDAO**

HIVI karibuni Rais John Magufuli, analikabidhi Jeshi la Magereza jukumu jipya, akiahidi kuliwezesha ili kuzalisha na kuwa kituo mahiri kitaifa cha kutafiti na kuzalisha mbegu zinazotumiwa nchini.

Ni taarifa njema ambayo pengine kwa miongo mitatu ilipasua vichwa wakulima na walinda mazingira na afya kwa sababu hakukuwa na jibu kuhusu hofu ya kuwapo mbegu zinazobadilishwa nasaba nchini.

Maamuzi hayo ya Rais yanapokelewa kwa moyo mkunjufu kutokana na ukweli kuwa, kampuni za kigeni zinazozalisha mbegu zimekuwa zikihofiwa kuhusishwa na kusambaza mbegu zilizofanyiwa mabadiliko ya vinasaba maarufu kama GMOs kwa mbinu wanazozijua wenyewe.

GMOs ambacho ni kifupisho cha maneno ya kitaalamu 'Genetically Modified Organisms' ni viumbe hai iwe mimea, wadudu au wanyama wanaozalishwa kwa kutumia uhandisi jeni au 'genetic engineering' unaobomoa na kurekebisha maumbile ya asili ya nasaba ili kukipa kiumbe kipya kinachotengenezwa sifa au tabia za ubora zaidi, lakini cha kushangaza kwa kutumia bakteria au virusi kupata mmea bora.

Bakteria au virusi hao huingizwa kwenye seli au chembe hai za mmea ili kuhamisha sifa 'bora' zinazotakiwa kwenye kiumbe kipya. Mara nyingi kinachowahofisha watu ni matumizi ya bakteria au virusi vinavyotumbukizwa ndani ya seli na nasaba za mmea ili kupata sifa zinazohitajika.

Ni ukweli kwamba binadamu hawataki kuhusishwa na bakteria na virusi popote iwe kwenye vyakula au kwa hali yoyote ile, ikizingatiwa kuwa leo dunia imesimama kutokana na kirusi cha corona kinachosambaza homa ya COVID-19 inayoshambulia mapafu na kuua kwa kasi.

Ndiyo maana wengi wanadhani kuwa GMOs ni mbaya na ni hatari si kitu cha kukimbilia. Lakini, wapo watetezi wa viumbe waliobadilishwa nasaba wanaosema hata leo hakuna athari zilizoonekana kwa binadamu zilizotokana na matumizi ya bidhaa za GMO.

Matumizi ya sayansi na teknolojia kwenye kuzalisha bidhaa zikiwamo mbegu yanahusishwa na udanganyifu na hata uwekaji wa vitu hatari kwenye vyakula ambavyo vinaweza kuathiri maisha na kusababisha magonjwa mathalani saratani, ndiyo maana serikali inapolipa Jeshi la Magereza jukumu hilo ni ukombozi kwa taifa.

Mathalani, Marekani ni nchi iliyombali kwenye matumizi ya GMOs na kwamba mazao yanayooteshwa ni pamoja na maharage ya soya na mahindi ya njano na yanaelezwa kuwa yanastawi hata pale dawa za magugu kama 'Monsanto's roundup' zinaponyunyizwa kwenye mashamba.

Cha kujiuliza inakuwaje mmea uendelee kukomaa na kuwa na sugu kwenye kemikali yakiwamo dawa ya magugu.

Serikali imefanya vyema kulipa jeshi hilo jukumu kwa kuwa mbegu za GMO zinazoelezwa kuwa zinaoteshwa mara moja na zikioteshwa mara ya pili baada ya kuvunwa hazioti wala haziweza kuzaa mara nyingine kwa sababu ya kutumia teknolojia ya kuharibu nasaba na jeni ya asili teknolojia inayoitwa 'gene terminator'.

Kuua uasili wa mmea hasa jeni au terminator gene' ndiko kunakozifanya mbegu kuwa tasa, kushindwa kuzalisha na kuendeleza tabia za asili za maumbile hali inayowalazimisha wakulima kununua mbegu kila msimu na ndicho kinachozifanya mbegu za GMO kuwa mzigo.

Lakini kuna maelezo kuwa mimea ya GMO inaposhambuliwa na visumbufu huviua, ikimaanisha kuwa wadudu wakiubungua hufa na swali linabaki kuwa kama panya, bungua na pekecha wanapokula mazao yao hufa vipi binadamu?

Hofu inabakia kuwa ni hatari kwa binadamu huenda kikawa chanzo cha saratani, ndiyo maana taifa kuwa na chombo chake cha kuzalisha mbegu ni muhimu hasa zama hizi za sayansi na teknolojia ya hali ya juu.

Mbali na maswali hayo ya kiikolojia kuna suala la kampuni zinazozalisha mbegu hizo kukandamiza wakulima wadogo hasa wa mataifa maskini kwa kutumia msuli wa fedha na kuwafanya wategemezi wa mbegu na viuatilifu vyao, hivyo endapo Tanzania inajitegemea kimbegu ni rahisi kuondokana na mkondo huo wa unyanyasaji.

Lakini, kampuni hizo za mbegu ambazo zina fedha nyingi na ukwasi wa kutisha zinahusishwa na kuingilia mitandao ya intaneti na kuondoa au kudhibiti taarifa zote zinazowazungumzia vibaya au kuhoji mienendo yao na wakati mwingine wametuhumiwa na kuwakwamisha walaji au wateja wanaotaka kuchokonoa na kujua zaidi habari za kampuni hizo hasa zinazohusu athari na usalam wa GMOs na matumizi ya kemikali mfano dawa za kuua magugu na nyasi mashambani.

Suala ambalo linaonekana sehemu nyingi duniani leo ni kupiga vita au kupuuza matumizi ya mbegu za asili ambazo zinaelekea kutokomezwa na nafasi yake kuchukuliwa na zinazozalishwa na kampuni za kimataifa zinazofanya tafiti, kuzalisha na kusambaza mbegu duniani ambazo ni pamoja na Monsanto la Marekani.

Kwa ujumla ni vyema kuwa na teknolojia za chakula na uzalishaji mbegu za ndani ya nchi kuliko kutegemea utafiti wa kigeni kwa sababu kinachoonekana ni kutaka uzalishaji wa haraka, wa taji , wa gharama dndogo na unaotumia eneo dogo kupata mazao mengine kwa kutumia teknolojia ambazo huenda ni hatarishi.

Utafiti unaofanywa na kampuni zinazozalisha mbegu za GMOs zama hizi unalenga kupata mbegu ambazo ni himilivu kwa ukame na zinazostawi bila hata kuhitaji mbolea. Mojawapo ni mahindi yanayostawi kwa tumia maji kiduchu (drought-resistant corn) hata hivyo, mbegu hizo hazijawa na mwitikio mkubwa. Uzalishaji huo umewahusisha wataalamu wa nchi za Afrika Kusini na Mashariki.

Hivi karibuni nchini Argentina utafiti ulijikita kwenye kuzalisha maharage ya soya yanayohimili ukame hata hivyo hakujawa na mafanikio kwa sababu watafiti hawajapata vibali wala leseni za kuzalisha mbegu hizo.

Baadhi ya taarifa zilizoko kwenye jarida la science journey, ni zile zinazozungumzia kazi ya shirika la kimataifa la International Maize and Wheat Improvement Center (CIMMYT) kwamba limeanzisha kituo cha kuhifadhi mbegu (seed bank) lengo likiwa ni kuzifanyia maboresho ili kuzalisha jamii inayohimili ukame na inayozaa sana.

Iwapo Tanzania itafanikiwa kujipatia mbegu zake yenyewe zinazozalishwa na Magereza itakuwa ni ushindi na ukombozi wa kuishi kwenye dunia hatarishi ambayo imejaa hofu kuwa hata magonjwa hatarishi yanayotokana na virusi kama COVID-19, SARS, kifua kikuu sugu ni matokeo ya kazi za maabara zinazofanywa na mataifa yenye teknolojia za hali ya juu kiwamo ya tiba na kilimo.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mkoa ulivyounda mabaraza vijiji, kukomesha ubakaji, ndoa utotoni



Mwenyekiti wa Baraza la Watoto la Kijiji cha Shilabela, Jessica Duma, aliye mbele ya wenzake. **PICHA: MARCO MADUHU**

WILAYA ya Shinyanga ni miongoni mwa halmashauri zinazokabiliwa na tatizo la mimba na ndoa za utotoni zinazowatumbukiza mabinti kwenye ujauzito na ndoa wakati walitakiwa kuwa shuleni.

Takwimu za kitaifa za mwaka 2012, zinaitaja Shinyanga kuwa mkoa unaongoza kwa mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora iliyokuwa na asilimia 58 na wa tatu ni Mara uliokuwa na asilimia 55.

Licha ya serikali na wadau kufanya juhudi mbalimbali za kutokomeza tatizo hilo kwa kushirikiana na mashirika watetezi wa haki za watoto, bado jamii zinahitaji kubadilika.

Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hilo Wilaya ya Shinyanga, inaunda mabaraza ya watoto ngazi ya kijiji ili kuongeza nguvu ya kupambana na kutokomeza matukio hayo ya ukatili dhidi ya watoto yanayohusisha mimba na ndoa.

Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008, ndiyo msingi kwa vile imeuainisha utaratibu wa kuanzishwa mabaraza hayo kwa ngazi mbalimbali.

"Mabaraza hayo ni sehemu ya utekelezwaji wa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, hasa ibara ya II kifungu cha 11, kinachosisitiza umuhimu wa haki ya mtoto katika kujenga hoja na kutoa maoni."

Pia kifungu hicho kinaelezea haki ya mtoto kusikilizwa na kushiriki kikamilifu katika mambo yanayohusu ustawi wake bila ya kikwazo, hivyo mabaraza hayo ya watoto ni chombo muhimu cha kuongeza nguvu ya kupambana na matukio ya ukatili na uhalifu dhidi yao.

Katibu wa mpango mkakati wa serikali wa kitaifa wa kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA), Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omari, anasema uundaji mabaraza hayo vijijini, utasaidia upatikanaji taarifa mapema kuhusu matukio ya ukatili kabla ya kuleta madhara.

Anasema watoto ni wepesi kupeana taarifa wao wenyewe zinazohusu matukio ya ukatili kupitia viongozi wa mabaraza hayo, kuliko kumwambia mtu mzima.

"Ni kwa sababu hawaogopani wala kuogopa kuambiana kama kuna mwenzao anafanyiwa ukatili kila siku, ama kupangiwa njama za kuozwa utotoni. Halmashauri yetu imeanza kuunda mabaraza vijijini na baadaye tutafika kwenye kata na wilaya ili kuwajengea uwezo watoto namna ya kupambana na vitendo vya ukatili wao wenyewe kwa kutoa taarifa mapema kwa viongozi wa serikali ili nasi tuchukue hatua," anasema Aisha.

Anaongeza: "Matukio ya ukatili ambayo tunapambana nayo sana katika halmashauri yetu ni mimba na ndoa za utotoni na kulazimisha wasichana kuacha shule."

Aidha, anasema wameshaanza kupokea taarifa juu ya vitendo vya ukatili ambavyo wanafanyiwa watoto, kupitia kwa viongozi wao wa mabaraza, ambapo kuna baadhi wameeleza kuzuiliwa kwenda shule, ili kwenye mitihani yao wasifanye vizuri ili waolewe.

"Baada ya kupokea taarifa hizi tutatuma maofisa ustawi wa jamii kwenda kwenye kaya hizo ili wazungumze na wazazi na kuwaonya kuhusu vitendo hivyo vya kuzuia mabinti wasiende shule na wakiendelea tutawachukulia hatua kali za kisheria," anafafanua Aisha.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Shilabela Kata ya Pandagichiza wilayani Shinyanga, Emmanuel Magadula, anasema uundwaji wa mabaraza hayo utafanikisha upatikanaji taarifa, ufuatiliaji mapema na udhibiti.

Anasema matukio mengi ya ukatili ambayo wamekuwa wakifanyiwa watoto wamekuwa hawapati taarifa mapema, bali husikika pale mtoto anapokuwa ameshadhurika, ikiwamo kupewa ujauzito ama kuingizwa kwenye ndoa na ameshatoroshwa na kuacha masomo.

Anasema tatizo hilo linatokana na utamaduni kuwa mtoto wa kike hana sauti ndani ya jamii ndiyo maana hata wakikutana na watu wanaowalaghai ama kuwafanyia ukatili hawezi kusema hadi anapata madhara.

"Sisi Serikali ya Kijiji cha Shilabela tunaamini kupitia viongozi wa mabaraza haya ya watoto, tutakuwa tunapata taarifa mapema kabisa juu ya vitendo vya ukatili ambavyo wanafanyiwa watoto, na tuta dhibiti mapema kabla ya kuleta madhara, na kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake kwa mujibu wa sheria na sera za watoto,"anasema Magadula.

Deogratius Mashamba ni Mtendaji wa Kata ya Pandagichiza Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, anasema taarifa nyingi za matukio ya ukatili dhidi ya watoto ambazo wamekuwa wakizipata, ni zile ambazo mtoto ameshafanyiwa madhara na kuwataka watumie fursa ya mabaraza hayo, kutoa taarifa za vitendo vya ukatili ambavyo wanafanyiwa ndani ya jamii, ili viongozi wao wafikishe taarifa hizo kwa viongozi wa serikali na zifanyiwe kazi na kudhibitiwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Watoto la Kijiji cha Shilabela, Jessica Duma, ambaye amechaguliwa na watoto kijijini humo, anasema baraza hilo litakuwa ni chachu ya mabadiliko kwa watoto katika kutetea haki zao kwa mujibu wa sheria zinazomlinda mtoto.

Anasema watoto wengi wamekuwa wakifanyiwa ukatili kijijini humo, lakini walikuwa hawana elimu ya wapi pa kutolea taarifa, lakini kupitia baraza hilo watalitumia vyema kupaza sauti juu ya matukio ya ukatili, ikiwamo ya upangaji njama za kumwozesha mwanafunzi, kwa kuanza kumzuia kwenda shuleni, ili afukuzwe ama afanye vibaya mtihani.

"Mimi ni Mwenyekiti wa Baraza la Watoto la Kijiji cha Shilabela, naahidi kushirikiana vyema na wenzangu, ili tupate taarifa juu ya vitendo vya ukatili ambavyo wanafanyiwa wenzetu, na tutazifikisha haraka sana kwa viongozi ili kufanyiwa kazi," anaongeza.

Mratibu wa mradi wa kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto kutoka Shirika la Rafiki SDO George Nyanda, anasema ni miongoni mwa wadau wa kutetea haki za wanawake na watoto mkoani Shinyanga, ambao kwa sasa wanatekeleza mradi wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, na wameamua kufadhili uundwaji wa mabaraza hayo ya watoto ngazi ya kijiji.

Anasema wameamua kushirikiana na serikali kuunda mabaraza hayo ya watoto, ili kuongeza nguvu ya mapambano ya kupinga matukio ya ukatili dhidi ya watoto, ikiwamo kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, tatizo ambalo limekuwa sugu kuisha.

"Sisi ni wadau wa maendeleo mkoani Shinyanga, kupitia Shirika letu la Rafiki SDO, tunaungana na serikali kuunda mabaraza haya ya watoto ngazi ya kijiji, kwa kushirikiana na Shirika la Women Fund Tanzania (WFT), ili kuongeza nguvu ya mapambano ya kutokomeza ukatili dhidi ya watoto, kwa kupaza sauti zao wao wenyewe,"anasema Nyanda.

Anasema viongozi wa mabaraza hayo watakuwa ni mabalozi kwa wenzao kupinga matukio ya ukatili, sababu wapo karibu muda wote, wakicheza ama kwenda kuchota maji na kazi nyingine, hivyo ni rahisi kupeana taarifa endapo kuna mwenzao anafanyiwa ukatili.





# Bodi ya Tumbaku kuongeza uzalishaji

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

BODI ya Tumbaku (TTC) imejipanga kuongeza uzalishaji wa zao la hilo, ili kukidhi mahitaji ya soko la dunia kutoka kilo 1,400 kwa hekta hadi kufikia 1,900 ili kuwainua wakulima kiuchumi.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Stanley Mnozya, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na mikakati waliojiwekea kuhakikisha zao hilo linaongeza pato la taifa na kuwainua wakulima.

Mnozya, alisema lengo lao ni kuona wakulima wa zao hilo wananufaika, lakini taifa linanufaika kupitia pato ambalo litaongezeka kutokana na uzalishaji huo.

"Moja ya mikakati ambayo bodi imejiwekea ni pamoja na kuhakikisha wanaongeza uzalishaji wa zao hilo la kimkakati nchini ambapo mkulima naye atainuka kiuchumi," alisema Mnozya.

Alisema mkakati mwingine ambao wamejiwekea ni pamoja na kuhakikisha wanaongeza ubora kutoka asilimia 93 hadi 97 ikiwemo kufanya marekebisho ya sheria ili ziendane na wakati.

Alisema hayo ni moja ya majukumu ambayo wamejipanga kuyatekeleza katika msimu wa 2020/2021 ili kuhakikisha wanafanikisha kile ambacho Bodi imepanga kukitekeleza katika msimu huu.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema wamejipanga kusimamia ipasavyo utunzaji wa mazingira kwa kuhimiza wakulima kupanda miti na kuboresha mabani ya kukaushia tumbaku.

Alisema ili kuhakikisha kuwa mafunzo kwa watumishi yanafanyika kama inavyotakiwa kwa ajili ya kuleta ufanisi zaidi katika zao hilo, Bodi imeanzisha mashamba darasa ili kutoa elimu ya uzalishaji bora na wenye tija kwa wakulima.

Alisema wanaamini mashamba darasa ambayo yatakuwa yameanzishwa yatasaidia kutoa elimu kwa wakulima wanaolima zao hilo hali itakayosaidia kusonga mbele katika kilimo hicho.

Alisema katika kuhakikisha wanafanikisha hilo, mashamba hayo yataunganishwa na maofisa ugani wa halmashauri, ushirika na kampuni kwa ajili ya kuwapa mafunzo ya kusimamia zao hilo ambao nao watakuwa wakitoa elimu kwa wakulima hao.

Akizungumzia kuhusu shughuli ambazo zimetekelezwa na bodi hiyo katika kipindi cha 2015/2016 hadi 2020/2021 ni kusajili wakulima wa tumbaku kisheria kwa sababu kabla ya kulima zao hilo waapaswa kusajiliwa na bodi na taarifa huingizwa kwenye mfumo wa wakulima.

# Maelfu ya wazee Kondoa wapatiwa vitambulisho

**Na Renatha Msungu, KONDOA**

HALMASHAURI ya Mji wa Kondoa imewatambua wazee 4,000 kati ya 5,000 ambao wamepatiwa vitambulisho ambavyo vitawasaidia kupata huduma mbalimbali ikiwamo matibabu.

Aidha, zoezi la upigaji picha kwa wazee linaendelea ili kupata idadi ya wazee waliopo katika maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa, Msoleni Dakawa, alisema wazee ni hazina kubwa, hivyo wanapaswa kuthaminiwa kutokana na kuwa na mchango mkubwa katika taifa.

Kutokana na hilo alisema serikali kila mara inafanya jitihada kujua takwimu zinazohusiana na idadi ya wazee kwa ajili ya mipango ya maendeleo.

"Kata ya Kingale imeonyesha kuwa na wazee wengi ambao wamefikia asilimia 90," alisema Msoleni.

Alisema kila mtu mwenye umri wa miaka 60 na kuendelea ana haki ya kuwa mjumbe kwenye baraza la wazee bila kujali itikadi za vyama, kabila wala dini.

**"Serikali imeweza kubaini takwimu zinazohusiana na idadi ya wazee kwa ajili ya mipango ya maendeleo, ambapo Halmashauri ya Mji Kondoa ina jumla ya wazee 5000 kati yao wazee 4,000 wametambuliwa na kupewa vitambulisho," alisema Msoleni.**

Hata hivyo aliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuhakikisha mpango wa uanzishwaji wa mabaraza ya wazee katika nchi ambao umewezesha upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati kuanzia ngazi ya mtaa na Taifa kwa ujumla.

"Serikali imeweza kubaini takwimu zinazohusiana na idadi ya wazee kwa ajili ya mipango ya maendeleo, ambapo Halmashauri ya Mji Kondoa ina jumla ya wazee 5000 kati yao wazee 4,000 wametambuliwa na kupewa vitambulisho," alisema Msoleni.

Pia alisema serikali imejitahidi kuhakikisha kunakuwa na huduma za msingi kama vile matibabu bure vinapatikana muda wote kwa ajili ya wazee na kuahidi kufanyia kazi changamoto ya upatikanaji wa dawa.

Mwenyekiti mteule wa baraza la wazee, Mohamed Majala, aliwataka viongozi waliochaguliwa pamoja na wazee wote katika baraza hilo kufanya kazi kwa ushirikiano ili kwa pamoja waweze kutimiza nia ya serikali ya kuwaleta wazee wote pamoja.

"Vijana mna mambo mengi ya kubuni tofauti na sisi wazee tunaishi kwa historia sasa, katika kujua mambo mengi sisi hatujui ila tutayajua mambo mengi kupitia kwa wazee wenzangu na vijana hivyo tushirikiane na kupitia mabaraza haya tunaomba tupate miongozo ya jinsi ya kuyaendesha haya mabaraza," alisema Msoleni.

Hafla ya uzinduzi wa baraza la wazee ilienda sambamba na kuchagua viongozi lengo ikiwa ni kuleta mabadiliko katika mabaraza yanayohusiana na wazee kama ilivyo kwa mujibu wa sheria na sera ya wazee ya 2003.



Ofisa Masoko Jiji la Dodoma, James Yuna, akizungumza na wawakilishi wa viongozi wa Machinga jana, kwa ajili ya kuwataka wafanyabiashara ndogo kushirikiana na halmashauri hiyo kwa kutowataka kufanya biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi na utunzaji wa mazingira. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mchungaji aondoa hofu ya Covid-19

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WATANZANIA wametakiwa kutekeleza maagizo ya Rais John Magufuli, ya kufanya kazi kwa bidii ili kuinua uchumi, badala ya kuendelea kuwa na hofu na mlipuko wa homa kali ya mapafu (COVID-19).

Aidha, wananchi wameshauriwa kutosikiliza kelele na vitisho vinavyotolewa na mataifa ya nje juu ya hali ya ugonjwa huo bali kinachotakiwa kuchukua tahadhari huku wakifanya kazi.

Mchungaji Dk. Vangast Salumu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God Upendo Rivival Christian Centre -TAG mkoani Dodoma alibainisha hayo jana, alipokuwa akizungumza na waumini wake.

Dk. Salumu alisema kuwa Watanzania katika kipindi hiki kiwe ni cha kufanya kazi kwa nguvu zote, na siyo wakati wa kusikiliza makelele na vitisho vinavyotolewa na nchi za nje.

Alisema kama Rais anavyohimiza kwa kututaka kufanya kazi na kumwamini Mungu, hakuna sababu ya kuwa na hofu bali kinachotakiwa kila mtu kujituma huku akichukua tahadhari na hali hiyo ya ugonjwa wa corona.

Alizitaka familia ambazo zina watoto wanaotakiwa kuanza masomo ya shule ya msingi na wale waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza wahakikishe wanawapatia haki yao ya msingi ya kusoma.

Alisema, serikali imewatua mzigo wazazi na walezi wenye watoto kwa kuwapunguzia makali ambayo yaliyokuwa wakikwamisha familia zilizo nyingi kutowapeleka shule kutokana na michango mbalimbali.

Dk. Salumu pia aliwataka waumini wa kanisa hilo pamoja na shughuli mbalimbali wanazozifanya za uzalishaji,wajikite kwenye kilimo na ufugaji kwa ajili ya kujipatia chakula cha kutosha.





# Serikali yaagiza wanaougua ugonjwa usiojulikana wapimwe

**Na Nebart Msokwa**

SERIKALI mkoani Mbeya, imeagiza Mganga Mkuu wa Mkoa huo kufuatilia na kuwasafirisha watu wote wanaodaiwa kuugua ugonjwa usiojulikana katika Kata ya Ifumbo, wilayani Chunya na kuwapeleka katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya ili wakapimwe na kupatiwa matibabu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alitoa agizo hilo juzi alipotembelea Kijiji cha Ifumbo akiwa na timu ya watalaamu wa afya kwa lengo la kujiridhisha kama ugonjwa huo usiojulikana ulioripotiwa kwenye vyombo vya habari kuwapo kwenye kata hiyo.

Baadhi ya wananchi waliopewa fursa ya kuzungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa kijijini hapo, walisema ugonjwa huo upo na umewasababishia wananchi wa kata hiyo madhara makubwa.

Mwenyekiti Mstaafu wa Kijiji cha Ifumbo, Elias Waya, alisema kwa mara ya kwanza ugonjwa ulionekana kwenye kata hiyo mwaka 1996 na ingawa wa walitoa taarifa serikalini, tatizo hilo halijawahi kushughulikiwa.

Alisema kwa kipindi hicho chote tatizo hilo limekuwa likiwasumbua, lakini mwaka jana liliwaathiri zaidi kwa kusababisha vifo vya watu 10 vilivyotokea kuanzia Aprili hadi Desemba.

"Ugonjwa huu ulikuwa ukiibuka kidogo kidogo na kutulia, lakini mwaka jana ulikuja kwa nguvu zaidi ukasababisha tukapoteza watu 10 hapa kijijini kwetu ambao wanawake walikuwa watatu na wanaume saba akiwamo mwalimu wa sekondari," alisema Waya.

Aliongeza kuwa tangu ugonjwa huo uibuke mwaka 1996, zaidi ya watu 34 walishapoteza maisha na mpaka sasa kuna wagonjwa zaidi ya 22 wanaougua ugonjwa huo kijijini hapo.

"Ukweli ni kwamba watu 34 waliofariki, hatuwezi kuwarekodi kwa vile walifia nje na mfumo wa 'record' (kumbukumbu) za afya, huku magonjwa ni mengi na tuko maeneo ya vijijini ambako hatupati ule muda mzuri wa kupima," alisema Chalamila.

Hata hivyo kwa wagonjwa ambao wanaendelea kuugua ugonjwa huo kijini hapo, alimuagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, kuwasafirisha bure kwenda katika hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya ili wapimwe na hatimaye wapate tiba.

"Inatakiwa wapelekwe hospitali ya rufani wakapimwe, nambieni hata kama wako 10, RMO awachukue awapeleke hospitalini wakapimwe, maana wakati mwingine mtu anaugua na hana hali nzuri ya kiuchumi," alisema Chalamila.

Aidha, alimtaka Mganga Mkuu wa Mkoa ikiwa yupo mtu aliyefariki kijijini hapo kwa ugonjwa huo, achukue sampuli kutoka kwenye mwili wa marehemu ili zikapimwe na kubaini aina ya ugonjwa uliosababisha kifo hicho.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, alisema amefikisha ombi maalum katika Wizara ya Afya ili itoe timu ya wataalamu kufika kijijini hapo kufanya uchunguzi wa kubaini aina ya ugonjwa huo kwa lengo la kupata tiba yake.

Taarifa za uwapo wa ugonjwa huo katika Kata hiyo ziliibuliwa mwishoni mwa wiki na madiwani wa Halmashauri Wilaya ya Chunya kisha kusambaa kwenye vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, alitoa taarifa za kukanusha huku akivishutumu baadhi ya vyombo vya habari kuwa vilitoa taarifa za kupotosha na akaagiza Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chunya kusimamishwa kazi.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Uhusiano iliyoko Kata ya Mwatenga, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakiendelea na shughuli za usafi wa mazingira kuzunguka maeneo mbalimbali ya shule hiyo, kabla ya kuruhusiwa kwenda nyumbani mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Polisi yawataka Mbarali kuanzisha sungusungu

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

JESHI la Polisi wilayani Mbarali, limewataka wananchi kuunda vikundi vya Ulinzi Shirikishi (Sungusungu) ili kukabiliana na vitendo vya uhalifu ikiwamo wizi wa mifugo.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Mbarali, Janeth Masangano, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa.

Alisema katika wilaya hiyo, limeibuka wimbi la vikundi vya watu wasiojulikana kuvunja nyumba za watu na kupora mali hasa nyakati za usiku na mchana wananchi wanapokuwa mashambani.

"Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiiba mifugo, wanachinjia kwenye vichaka na kuondoka na nyama, huku wakitelekeza baadhi ya viungo, sasa hili jambo linahitaji ushirikiano wa hali ya juu ili kukomesha uhalifu huu," alisema Masangano.

Aidha, alisema kuna baadhi ya viongozi wa vijiji na mitaa wamekuwa wakishirikiana na wahalifu hao kutekeleza uhuni huo na hivyo akawataka kuacha mara moja tabia hiyo kwa maelezo kuwa watakumbana na mkono wa dola.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na operesheni usiku na mchana katika kukabiliana na suala la wizi wa mifugo na uvunjifu wa nyumba, huku akiwaomba viongozi hao kuendelea na usafi wa vichaka ambavyo vinaficha wahalifu.

"Tuungane kukomesha vitendo hivyo, tunahitaji wilaya yetu iwe salama maana tunapokea wageni wa kila aina... kuna wafanyabiashara wa mazao na wakulima wanahitaji kufanya shughuli zao katika hali ya usalama," alisema Masangano.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji wa Rujewa, Chameta Godigodi, aliwaagiza wenyeviti kuacha tabia ya kuwakumbatia wahalifu na badala yake wawaripoti kwenye vyombo vya sheria ili kukomesha vitendo hivyo.

Mtendaji wa Mamlaka ya Mji huo, Tuntufye Chamba, aliwaomba wenyeviti pamoja na wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kukabiliana na vitendo hivyo.

## Mbeya-WSSA sasa kupanda miti 6,000,000

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani Mbeya (Mbeya-WSSA) imesema inakusudia kupanda zaidi ya miti 6,000,000 kwenye vyanzo maji ili kulinda na kutunza uoto wa asili kuzunguka maeneo hayo.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Stella Wadson, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe, na kusema wamejipanga kupanda miti 6,000,000 kwenye vyanzo vya maji ili kukabiliana uharibifu wa mazingira.

Alisema kumekuwapo na uvamizi kwenye vyanzo vya maji, na kwamba wanapanda miti ya aina mbalimbali ili kulinda visiharibiwe na wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

"Bado tunaendelea na upandaji miti, kwa mwaka huu tunakusudia kupanda miti 6,000,000 tutawashirikisha wadau na wananchi wa maeneo mbalimbali kupanda miti hiyo kwenye vyanzo vya maji," alisema Wadson.

Mamlaka hiyo imetoa rai kwa wananchi kuwa na uzalendo katika kuhifadhi rasimali za maji kwa ajili ya maendeleo endelevu kwa maisha ya watu na shughuli za uchumi.

Hivi karibuni, Jumuiya ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mbeya Mjini, ilisema kuwa ukosefu wa alama za kuonyesha mipaka kati ya vyanzo vya maji na makazi ya watu ni moja ya sababu zinazochangia migogoro baina ya vyanzo vya maji na wananchi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Afrey Nsomba, alisema walibaini hilo baada ya kupanda miti katika chanzo cha maji cha Mto Nzovwe, ambapo baadhi ya viongozi wa chama hicho walisema ukosefu wa alama za mipaka unachangia kuaathari uhifadhi.

Alisema chanzo cha maji cha Mto Nzovwe kilichopo Kata ya Mwakibete ni moja ya vyanzo muhimu kwa wakazi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, lakini kinakabiliwa na tatizo la uvamizi wa makazi ya watu yanayotishia usalama wa chanzo hicho.

Alidai zaidi ya miti 2,000 ilipandwa na Jumuiya ya Wazazi ya CCM Mbeya kama jitihada za kuhifadhi na kurejesha uoto wa asili katika maeneo yaliyoathiriwa na uvamizi wa shughuli za kibinadamu.



## SMZ yajivunia kipaumbele cha masuala ya jinsia

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Abeda Rashid, amesema serikali ya Zanzibar, imeonyesha nia nzuri ya kutoa kipaumbele katika masuala mbalimbali yanayozingatia jinsia.

Rashid alisema miongoni mwa mambo ambayo serikali ya awamu ya nane imeanza kuonyesha nia njema ni pamoja na kutoa nafasi mbalimbali za uongozi kwa wanawake.

Aliyasema hayo katika mkutano wa kufunga mradi wa wanawake ambao ulikuwa ukisimamiwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA) uliofanyika mjini Zanzibar.

Rashid aliitaka jamii kuithamini nafasi ya mwanamke na pia kuwataka wanawake hao kujitathmini wenyewe na kujitambua.

Alishauri kuwapo kwa taratibu, sera na sheria kwa vyama vya siasa ambazo zitavibana vyama hivyo navyo kutoa nafasi kwa mwanamke bila ya ubaguzi ikiwamo kuwasimamisha kuwania nafasi mbalimbali na katika majimbo ya uchaguzi.

"Lazima kuwawekea mazingira rafiki wanawake ambapo, ni vema wakisimama tuwape ushirikiano mkubwa," alisema Naibu Katibu Mkuu huyo.

Alisema kuwa mradi wa wanawake sasa umeleta mafanikio makubwa ikiwamo kuwasaidia wanawake hao kujitokeza kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana na kuomba mradi huo kuendelea ili kuleta hamasa kwa idadi kubwa ya kundi hilo kuingia katika uongozi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Reuben, alisema mradi huo umeleta mafanikio mazuri na kwamba wanawake wanasiasa 150 walijifunza umuhimu wa kutumia vyombo vya habari na kueleza ajenda zao za kisiasa kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Pia alisema wanawake hao walijifunza changamoto katika mlengo wa ukatili wa kijinsia ikiwamo namna ya kupambana na rushwa ya ngono.

Kwa upande wake Mjumbe wa Kamati ya Amani Zanzibar, Shekhe Fadhila Suleiman Suraga, alisema wanawake wanapopata nafasi za uongozi hufanya vizuri katika utendaji wao na huonyesha utayari katika kutafuta ushauri kutoka kwa watu wengine na kwamba ni vema kuendelea kuwaunga mkono.

> **"Lazima kuwawekea mazingira rafiki wanawake ambapo, ni vema wakisimama tuwape ushirikiano mkubwa," alisema Naibu Katibu Mkuu huyo.**

# Baraza la Wawakilishi lataka subira kutathmini utendaji kazi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

BARAZA la Wawakilishi Zanzibar limesema bado ni mapema kutathmini utendaji wake katika kusimamia serikali ya awamu ya nane ambayo inaonyesha kuwa na kasi ya utendaji na uwajibikaji kwa siku za mwanzo tangu ilipoingia madarakani hususani katika kupambana na vitendo vya rushwa na ufisadi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Idara ya Ushauri, Sheria na shughuli za Baraza la Wawakilishi, Mussa Kombo Bakari, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano wa pili wa Baraza la 10 la Wawakilishi unaotarajiwa kuanza leo.

Alisema kamati za kudumu za baraza hilo wajibu wake mkubwa ni kufuatilia miradi mbalimbali ya serikali na kutoa mapendekezo na hazina mamlaka ya kukamata au kushtaki.

"Ni mapema kutoa tathmini ya baraza katika mtazamo wa kuendana na kasi ya uwajibikaji iliyoanzishwa na serikali ya awamu ya nane, lakini kamati za kudumu za baraza zimeanza kufanya kazi na zinatarajiwa kuwasilisha ripoti zake katika mkutano ujao," alisema Bakari.

Alisema kutokana na mfumo wa katiba wa kuwapo serikali ya umoja wa kitaifa, Baraza halitakuwa na kambi ya upinzani badala yake kutakuwa na serikali na wajumbe wa baraza kutoka vyama tofauti vya siasa.

Akiwasilisha ratiba ya mkutano huo, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Mselem, alisema wajumbe wanatarajia kupokea na kujadili ripoti mbalimbali za kamati za kudumu ikiwamo ripoti ya nne ya utekelezaji wa kazi ya tume ya maadili ya viongozi wa umma ya mwaka 2019/2020.

Ripoti nyingine inayotarajiwa kujadiliwa na wajumbe hao ni ripoti ya Mdhibiti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Wizara mbalimbali, mashirika, Serikali za Mitaa ya mwaka 2018/2019 na ripoti ya jitihada za kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar ya mwaka 2020.

Pia alisema kazi nyingine zitakazofanyika katika mkutano wa baraza hilo la 10 ni marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar Namba 4 ya mwaka 2015, pamoja kujadili hotuba ya Rais wa Zanzibar ya ufunguzi wa Baraza la hilo, mwelekeo wa mpango wa taifa wa mwaka 2021/2022, muswada wa dharura wa sheria ya mambo mbalimbali, uchaguzi wa wenyeviti wa baraza na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mselem alisema maswali 91 yanatarajiwa kuulizwa na kujibiwa na serikali na kwamba katika mkutano huo, wajumbe watano kutoka Chama cha ACT-Wazalendo wataapishwa.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, akiongoza matembezi ya Siku ya Sheria Zanzibar yaliyoanzia majengo ya Mahakama Kuu Vuga na kumalizia Viwanja vya Maisara kupitia Michenzani na Kariakoo. **PICHA: IKULU**

# Makamu wa Rais ashauri siku maalum ya kuendesha baiskeli

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, ameshauri kuwapo siku maalum ya uendeshaji wa baiskeli ili kujenga utamaduni kwa jamii kupenda kufanya mazoezi hayo kwa ajili ya kujenga afya zao.

Alisema licha ya uwapo wa vikundi vya mazoezi katika maeneo mbalimbali, lakini bado asilimia kubwa ya wananchi hawana utamaduni wa kufanya mazoezi.

Hemed alizitaka manispaa na halmashauri kutenga siku maalum ya kuwahamasisha wananchi kutembea kwa lengo la kurejesha utamaduni wa asili wa watu kupenda kutembea ambao kwa sasa uko hatarini kupotea kutokana na kuongezeka kwa vyombo vya moto.

Hemed alisema ni vema jambo hilo likaenda sambamba kwa manispaa na halmashauri hizo kutunga sheria ndogo zitakazolinda maeneo na njia za watembea kwa miguu bila ya kuingiliwa na shughuli zengine.

"Si jambo baya kwa mamlaka zetu za miji kutunga sheria ndogo zitakazohamasisha wananchi kutumia baiskeli pamoja na kuwalinda wapanda baiskeli kiusalama," alisema Hemed.

Alieleza kwamba taifa likiendelea kubaki na watu wenye afya bora na wenye kuongeza ufanisi katika kazi, bajeti ya serikali kupitia wizara inayosimamia sekta ya afya ya kuagiza dawa nje ya nchi inayogharimu fedha nyingi za kigeni itapunguwa.

Aliwataka watendaji wa taasisi za umma wakiwamo mahakama wanaotumia muda mwingi kukaa maofisini kutenga muda maalum kulingana na mazingira yao ya kazi kwa ajili ya kufanya mazoezi kwa ajili ya kulinda afya zao.

Naye Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, alisema umbali wa matembezi ya mwaka huu ambao ulikadiriwa kuwa ni kilomita tatu umetoa fursa ya washiriki wote kumaliza matembezi hayo.

Alisema tayari uongozi wa Mahakama Zanzibar umefikiria wanasheria kuwa na utaratibu wa kuanza kufanya mazoezi kila mwezi kutokana na kutumia muda mwingi kukaa ofisini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAJENGO YA MAGHOROFA YANAUZWA DAR:

**Sasa wasiliana na Madalali Makini wa Dar (MAMADAR) kununua Majengo ya Maghorofa Dar. Wapigie Simu: 0714 564651 / 0759 848155**

## MAENEO MAZURI KWA AJILI YA KUJENGA SHELL (PETROL STATION) YANAUZWA:

**Wasiliana na Tanlands Real Estate Agency (TREA). SIMU: 0759 848155 / 0745 312893..**

## KISEMVULE!! KISEMVULE!! VIWANJA VINAUZWA KISEMVULE:

**Vipo karibu na Barabara kubwa. Wasiliana na Kisemvule Pazuri Group (KPG). Simu No: 0713 256904 / 0714 564651**

## MAGODOWN YANAUZWA / YANAPANGISHWA DAR:

**Kwa mahitaji ya kununua / kupangisha Magodown Dar. Wasiliana na Madalali Makini wa Dar. SIMU: 0714 564 651 / 0759 848 155**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA MWANZO (W) YA IRINGA MJINI WILAYA YA IRINGA**

**SHAURI LA NDOA 6/2021**
**MDAI: CATHERINE D/O MLOWE WA IRINGA**
**MDAIWA: BENJAMINI S/O MBAWALA WA SIMIYU**

KWAKUWA MDAI AMELETA MADAI YAKE YA KUACHANA NA MDAIWA KWAHIYO UNAHITAJIKA KUHUDHURIA BINAFSI KATIKA TAREHE 1/3/2021 SAA 2.30 ASUBUHI KWA SHAURI HILO NI LAZIMA KULETA MASHAHIDI WENU NA HATI ZOTE ZINAZOHUSU SHAURI HILO.
USIPOFIKA SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA.

**HATI HII IMETOLEWA LEO 5.2.2021**
**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KHALID HUSSEIN MUCCADAM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 786 AHG – NISSAN.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: DAR/MBU/RB/829124/2020.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

## OMBI LA URAIA WA TANZANIA



**MR. REDA KASSEM HODROJ**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, utaifa wake kwa sasa ni MLEBANONI nchi atokayo LEBANON shughuli zake ni MHANDISI-MITAMBO anwani ya mwajiri/biashara LUGOBA CHALINZE yupo nchini tangu tarehe 23/01/2008 pamoja na kuishi MSOLWA-CHALINZE mkoa wa PWANI, pia amewahi kuishi LUGOBA CHALINZE, Wilaya ya Bagamoyo mkoa wa PWANI. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, S.L.P 512 Dar es salaam. KUMB. NA. DN 514298.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI (TRAILER)

**BHESANIA GARAGE LIMITED P.O.BOX 253 IRINGA** tunatangaza kupotelewa na kadi ya gari (Trailer) lenye namba za usajili T936 AHQ. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Taarifa ya polisi RB. Namba IR/IR/RB/1263/2020.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA MAPITIO YA JINAI NA.2/2018**
**(Asilia Shauri la Jinai na. 90/2017, Mahakama ya Wilaya ya Lindi)**

**MKURUGENZI WA MASHTAKA ..............................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**SELEMANI AMRI MKOKOTOLE .......................MJIBU RUFANI**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA**
**SELEMANI AMRI MKOKOTOLE**
**NANGARU**
**LINDI**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMNA KUU MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 15/03/2021 SAA 2:30 BILA KUKOSA.
KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA , BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA WEWE KUWEPO.
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURUI WA **MAHAKAMA LEO HII TAREHE 2/12/2020.**

**A.H. MSUMI**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MTWARA**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BHESANIA GARAGE LIMITED P.O.BOX 253 IRINGA Tunatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya CALTIC yenye namba za usajili T706 AQK Lenye chassis namba LNJDGDE 1X6L518608 injini namba B6329188. KADI namba 982017. Taarifa ya polisi RB. Namba IR/IR/RB/1263/2020.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo MJINI**
**Wilaya ya MBEYA**
**MIRATHI 14/2020**

MDAI: **DEOGRATIUS REUBEN MASUBO**
MDAIWA: **MARIAM (ZUHURA KULWA MASUBO**
KWA: **MARIAM (ZUHURA KULWA MASUBO**
K.K: **GAZETI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
**KWA AJILI YA KUJITOA KWENYE ORODHA YA WANUFAIKA WA SHAURI LA MIRATHI NO. 14/2020 LA MAREHEMU KULWA REUBEN MASUBO**
Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe 01/03/2021 saa 2:30 Asubuhi/alasiri kwa kujibu madai haya na kwa kuwa hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalizo: Angalia kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 03/02/2021.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo MJINI**
**Wilaya ya MBEYA**
**MIRATHI 14/2020**

MDAI: **DEOGRATIUS REUBEN MASUBO**
MDAIWA: **AISHA RIDHIWAN LUOGA**
KWA: **NIABA YA NEEMA KULWA MASUBO**
K.K: **GAZETI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
**KWA AJILI YA KUJITOA KWENYE ORODHA YA WANUFAIKA WA SHAURI LA MIRATHI NO. 14/2020 LA MAREHEMU KULWA REUBEN MASUBO**
Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe 01/03/2021 saa 2:30 Asubuhi/alasiri kwa kujibu madai haya na kwa kuwa hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalizo: Angalia kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 03/02/2021.

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA ILEMELA**
**SHAURI LA MAOMBI NO. 14 OF 2020**
**(Linatokana na shauri asilia la ndoa No 18/2020 kutoka mahakama ya)**
**Mwanzo Ilemela**

**RAMADHANI CHEREHANI............................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ZAMDA HARUNA....................... MJIBU MAOMBI**
**KWA : ZAMDA HARUNA**
**P.O.BOX 1333**
**MWANZA**
**0742984410**
**AU POPOTE ALIPO TANZANIA BARA**

**KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa mdai amefungua shauri la maombi ya kukata rufaa nje ya muda na maombi yamepangwa kutajwa mbele ya Mh. A.N.SUMARI tarehe 12 mwezi Februari 2021,
Hivyo basi unatakiwa kuhudhuria bila kukosa au mwakilishi wako ili kusikiliza maombi tajwa hapo juu.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 5 mwezi Februari 2021.

.........................................
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA ILEMELA**

---

**ABA-JAJA COMPANY LIMITED**
**TAARIFA/NOTISI**

Katika Mahakama ya Mwanzo Kizumbi iliyopo Shinyanga

SHAURI LA MADAI NAMBA 120/2019
MAGANGA MAGULYA MAGANGA (Mdai)
SAADA RAMADHANI CHOOGERO
(Mdaiwa)

**Kwa: SAADA RAMADHANI CHOOGERO**
Unataarifiwa kuwa nimepewa hati ya kukamata mali dhidi yako katika shauri la Madai Namba 20 ya 2019 ya Mahakama ya Mwanzo Kizumbi iliyopo Shinyanga. Unataarifiwa kuwa ulipe Tsh. 700,000/= kwa ajili ya Mdai Maganga Magulya Maganga ndani ya siku kumi nan ne (14) za kazi tangia siku ya kutolewa kwa taarifa (Tangazo) hili pamoja na gharama za ukazaji hukumu. Usipotekeleza hatua nyingine za ukazaji hukumu zitaendelea dhidi yako bila taarifa (notisi) nyingine kutolewa kwako.

C. R. Kabenga
Dalali wa Mahakama
SHINYANGA

---

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

RIPOTI MAALUM-2

# MAAJABU YA WATOTO WENYE SARATANI

**Na Romana Mallya**

JANA katika sehemu ya kwanza ya ripoti hii tulionyesha jinsi ubunifu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kuwa darasa la kuwasaidia watoto wanaendelea na matibabu ya saratani licha ya vikwazo vya kiafya wanavyopitia, kusoma kama watoto wengine ili wanaporudi shuleni wasiachwe nyumba. Katika toleo la leo tunaona jinsi watoto hao walivyo na ndoto za kuwa madaktari ili asaidie wengine. Sehemu hii ya pili na ya mwisho inabainisha mengine zaidi...

Mwalimu Leonard Willium anayefundisha watoto hao, anasema kila mtoto ana ndoto yake na walio wengi wamejikuta wakizibadilisha hasa kutokana na kuwa muda mrefu hospitalini.

"Wengi wamekuwa wakitueleza kuwa wakifanikiwa kutoka salama hospitali na wakiwa wakubwa wanatamani kuwa madaktari na tunapowauliza sababu za kupenda udaktari hueleza kuwa wanaona watu wengi wanahitaji kupata matibabu," alisema.



Mwanzilishi wa Taasisi ya Tumaini la Maisha, Mwalimu Leonard William, akiwa na baadhi ya wanafunzi wake katika darasa la michezo lililoko jengo la watoto katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). **PICHA: ROMANA MALLYA**

**RATIBA YA MASOMO**

Mwalimu William alisema kila siku ikifika saa 3:00 asubuhi kuanza masomo, ambapo kwa saa moja baada ya kufika huitumia kwa michezo ambayo huicheza nje ya jengo hilo la watoto.

"Baada ya michezo, tunarudi darasani na tunatumia robo saa kuimba nyimbo za shule na tukimaliza watoto wanapumzika na kupata juisi maalum ambayo hutengenezwa hospitalini hapo na wakimaliza mapumziko hurejea darasani na kuanza masomo.

"Watoto wanafanya masomo kwa vipindi viwili, muda wa saa sita hadi saa saba kwa watoto wadogo huangalia katuni na kucheza michezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanga michezo ya herufi, namba au picha na wengine husoma masomo yao kulingana na madarasa yao."

**UELEWA WA MASOMO**

Mwalimu William alisema kuwapo kwa madarasa hayo kumewasaidia kisaikolojia watoto wao na maendeleo yao darasani ni mazuri.

"Tunavyojipima, wanapomaliza darasa la saba wapo waliofaulu na kuingia kidato cha kwanza, kwa hiyo tunaona kazi tunayoifanya kwao siyo bure, ina mafanikio kwao, tunapokea watoto wenye umri wa miaka mitatu hadi 20 na kwa sababu wanafahamu wapo kwenye matibabu hata wenye umri kuanzia sifuri wakati wa michezo wazazi wao huwaleta kushiriki," alisema.

Kuhusu changamoto, mwalimu William alisema hasa wanahitaji vitabu vya masomo mbalimbali pamoja na madaftari na 'tablet' za kujifunzia.

"Uhitaji wa vitabu ni vya darasa la tatu mpaka darasa la saba hasa vya hesabu, Kiswahili na Kiingereza," alisema.

**WANUFAIKA WANENA**

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Kizinga iliyopo Kizuiani jijini Dar es Salaam, Enock Mbwilo (14), ambaye yupo hospitalini hapo akiendelea na matibabu na kupata fursa ya elimu anasema Tumaini la Maisha limerudisha ndoto zao.

Mbwilo ni miongoni mwa wanufaika wakubwa wa elimu hiyo ambayo tangu akiwa na umri wa mwaka mmoja alikuwa akihudhuria masomo yanayotolewa katika madarasa yaliyopo ndani ya jengo moja la wodi za watoto.

Nikiwa na umri wa mwaka mmoja nililetwa hapa hospitali kwa ajili ya kuanza matibabu, wakati tupo wodini ndipo mzazi wangu alipoambiwa kuhusu madarasa haya, hivyo nilianza kuhudhuria tangu wakati huo na hata nilipofika umri wa kwenda shule nilikuwa nimejifunza vitu vingi," anasimulia.

Mbwilo anasema elimu anayoipata hapo inamwezesha kwa kiasi kikubwa kwenda sambamba na wenzake pindi anapoendelea na matibabu hospitalini hapo.

"Ninamshukuru Mungu nilianzia hapa hapa kusoma na nikajua kusoma na kuandika, nilianza masomo hapa nikiwa bado mdogo, nilipopata nafuu wakati huo na nilipofikisha umri wa kuanza shule wazazi wangu waliniandikisha shule.

"Kwa hiyo nimekuwa nikisoma shule mbili tofauti, nikiwa kwenye matibabu nasoma hapa na nikipata nafuu narudi kwenye shule ambayo nimeandikishwa."

Anasema usomaji huo umemsaidia kwa kiwango kikubwa kuweza kufanya vizuri darasani na katika matokeo ya mwaka jana (2020), alishika nafasi ya tatu darasani kwao na kupatiwa zawadi ya madaftari.

**WITO KWA WALIMU**

Mbwilo aliwataka walimu wake wa hospitalini hapo pamoja na shule anayosoma, wasife moyo waendelee kuwafundisha na Mungu awatia nguvu wakati wote wanapofundisha licha ya changamoto walizonazo.

"Ninawaambia walimu wangu Mungu awatie nguvu wazidi kutufundisha wala wasichoke na wanafunzi wenzangu wazidi kusoma kwa bidii, wazazi waendelee kutuuguza na madaktari waendelee kututibia wasichoke.

"Tunaomba watu watusaidie katika madarasa yetu hapa hospitali hatuna vitabu vya kutosha vya masomo mbalimbali, vya hadithi na vitu vya michezo hivyo wakiguswa watusaidie ili tunapokuwa darasani tuweze kusoma kama watoto wengine waliopo shuleni."

**NDOTO YA UDAKTARI**

Mwanafunzi huyo anabainisha kuwa siku hiyo (Februari 4) alisoma masomo mawili ya Hisabati na Kiswahili na masomo anayoyapenda ni Sayansi, Hisabati, Kiswahili na Geografia.

"Masomo ambayo sifanyi vizuri ni Kiingereza kwa sababu sikielewi. Nikiwa mkubwa ninataka kuwa daktari kwa sababu ndiyo kazi ninayoipenda," anasema.

Mbwilo anasema alirudi kwa matibabu hospitalini hapo Desemba 18, mwaka jana, hivyo mwaka huu alitakiwa kuingia darasa la sita.

"Ila kwa sababu hapa tuna madarasa wakati nikiendelea na matibabu nimekuwa nikihudhuria masomo ya darasa la sita. Ninamshukuru Mungu leo nimeruhusiwa hivyo ninarudi nyumbani kuendelea na shule, darasa hili limenisaidia sana kwa sababu nikisoma hapa nikirudi shule sioni kama kuna kitu kigeni ninaendelea na wenzangu," anasema.

Mtoto huyo anasema uongozi wa Muhimbili na taasisi hiyo wamefikiria jambo muhimu kwa kuamua kutoa elimu kwao wanayoipata ghorofa ya tatu kwenye jengo la watoto karibu na wodi zao ambapo hata mtoto akizidiwa darasani ni rahisi kurudi kwenye matibabu.

**MZAZI AFUNGUKA**

Nuru Shabani mwenyeji wa Manyoni, mkoani Singida ambaye yupo hospitalini hapo kwa ajili ya matibabu ya mtoto wake, analiambia gazeti hili kuwa hakutegemea kama ndani ya hospitali angekuta madarasa ambayo yanawasaidia watoto kuendelea kusoma masomo yao wanayojifunza shuleni.

"Mtoto wangu ana saratani ya tezi, kwa kule wilayani walijua ni Kifua Kikuu (TB) akawa anashindwa kupumua vizuri kwa sababu tezi lilikuwa linakandamiza mfumo wa upumuaji, alianza kuumwa tangu mwezi Septemba mwaka jana na ndiyo ilikuwa mwezi wake wa mwisho kuhudhuria darasani, yupo darasa la sita," anasema.

Kwa mujibu wa mzazi huyo, baada ya kufika hospitalini hapo na kubainika tatizo lake la ugonjwa, wakiwa hapo ndipo walipogundua kuna madarasa kwa ajili ya watoto wanaoumwa.

"Niliongea na mwalimu na sasa anahudhuria masomo ya darasa la saba ambapo tumeambiwa akirudi nyumbani ataendelea na masomo ya darasa la saba, programu hii ni nzuri kwa sababu wanapoumwa wapo wanaokata tamaa kwamba wenzao wanaendelea na masomo wao wapo tu kitandani wanaumwa, mwishoe wanakata tamaa kwamba hawatarudi shule.

"Wanapoendelea na masomo hapa wanapata moyo kwa sababu mtoto wangu alikuwa analia anasema wenzake wanaendelea na masomo yeye yupo hospitali lakini tulipogundua kuna masomo yanayofundishwa hapa sasa ana furaha," anasema.

Shabani anatoa wito kwa wadau mbalimbali wenye uwezo kujitokeza kusaidia zaidi huduma hiyo kwa kuchangia vifaa vinavyohitajika ili watoto hao wawapo kwenye matibabu wajione bado wapo shuleni.



# LEIPZIG, LIVERPOOL KUVAANA HUNGARY

**LONDON, England**

MJI wa Budapest utaandaa mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora kati ya RB Leipzig na Liverpool, UEFA imethibitisha.

Ratiba hiyo ililazimika kuhamishwa baada ya Ujerumani kuweka vizuizi vya kusafiri kwa kuingia kwa wanaowasili kutoka maeneo yaliyoathiriwa na mabadiliko ya corona hadi angalau Februari 17 siku moja baada ya mchezo huo kupigwa.

Vizuizi vipo kwa raia wa Ujerumani au wakazi, lakini hakuna kanuni maalum kwa wanamichezo wa kitaalamu, ikimaanisha kuwa kikosi cha Liverpool hakitaruhusiwa kuingia nchini humo.

Sheria zilizowekwa na UEFA zinaruhusu michezo 16-bora kubadilika au, vinginevyo, kuhamishiwa kwenye uwanja wa upande wowote.

Kwa kushirikiana na klabu zote mbili, baraza linaloongoza limetangaza Leipzig na Liverpool watamenyana katika Uwanja wa Puskas katika mji mkuu wa Hungary badala yake.

"UEFA inapenda kuwashukuru RB Leipzig na Liverpool kwa ushirikiano wao wa karibu na msaada katika kutafuta suluhisho la suala lililopo, na vile vile Shirikisho la Soka la Hungary kwa msaada wao na kukubali kuandaa mechi husika," taarifa kutoka UEFA ilisomeka hivyo.

Mchezo huo utabaki tarehe ya kwanza Februari 16, na mechi ya kurudiana itapigwa Machi 10, mwaka huu huko Anfield.




## IBRAHIMOVIC SASA AFIKISHA MABAO 500

**MILAN, Italia**

ZLATAN Ibrahimoic amefikisha mabao 500 kwa klabu baada ya kufunga bao la kwanza AC Milan ilipocheza dhidi ya Crotone.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, alifikisha rekodi ya mabao 499 Jumanne walipocheza dhidi ya mahasimu wao, Inter Milan katika michuano ya Coppa Italia.

Ibrahimovic alipaswa kufunga bao katika kipindi cha kwanza dhidi ya Bologna wikendi iliyopita, lakini alikosa penalti ya dakika ya 26, ingawa Ante Rebic alifunga bao hilo.

Lakini wakatiwa mafanikio kwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Sweden, ulifika San Siro wakati alicheza moja-mbili na Rafael Leao.

Kufurahia kwa mara ya pili na Milan sasa akiwa na umri wa miaka 39, mabao yake yameirudisha timu ya Stefano Pioli kwenye kinyang'anyiro cha ubingwa.

Rossoneri hawajashinda Scudetto tangu 2011 - katika msimu wa kwanza wa Ibrahimovic klabuni na hawana taji lolote tangu walipobeba Supercoppa Italiana mwaka 2016.

Kwa mchezo wa Jumapili, Ibrahimovic sasa ana mabao 15 katika mashindano yote msimu huu, pamoja na 13 kwenye ligi.

Ibrahimovic amekuwa mmoja wa majina makubwa ya mpira wa miguu Italia katika karne ya 21, lakini amethibitisha thamani yake ulimwenguni kati ya uhusika wake pale Serie A.

Na uhakika sehemu kubwa zaidi ya mabao yake 500 ilikuja akiwa na Paris Saint-Germain, 156 katika mechi 180 tu.

# KOEMAN AMSIFIA MESSI



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, amemsifia Lionel Messi kwa kubadilisha mchezo akitokea benchi na kuiwezesha timu yake kupata ushindi wa mabao 3-2 kwenye LaLiga dhidi ya Real Betis.

Messi alikuwa benchi kwenye mchezo huo kabla ya kuingia na kusawazisha kwa kuitoa safu ya ulinzi ya Betis, kwenye mchezo huo uliopigwa Jumapili.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, alifunga baada ya dakika 136 kuingia uwanjani, likiwa ni bao la haraka zaidi kufungwa kwa mtokea benchi kwa Barca kwenye LaLiga.

Trincao alifunga la ushindi dakika ya 87 kwa Barca, ambao wamepitwa pointi saba na vinara, Atletico Madrid, ingawa wana mechi mbili mkononi.

Koeman akasifia mchango wa Messi baada ya mchezo huo, akiwaambia waandishi wa habari: "Mara zote nazungumza na wachezaji na kuwaonyesha mawazo yangu.

"Nilizungumza na Lionel Messi jana kuhusu mchezo huu na kwamba atahitaji kwanza kupumzika na baadaye ningemwingiza na akafanya vile tulivyozungumza."

HABARI MICHEZO




# SOLSKJAER

## AKATA TAMAA UBINGWA EPL KWA UTD

**MANCHESTER, England**

KOCHA Mkuu wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameweka wazi kuwa matarajio yao si kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Kikosi cha United kimeonyesha kuimarika msimu huu ndani ya uwanja ambapo kimekuwa kikipata matokeo chanya ndani ya dakika 90.

Kauli ya Solskjaer imekuja baada ya kulazimishwa sare ya kufungana mabao 3-3 dhidi ya Everton ikiwa ndani ya Old Trafford ambapo United ilianza kufunga kupitia kwa Edinson Cavani dakika ya 24, Bruno Fernandes dakika ya 45 na lile la tatu la Scott Mc Tominay.

Everton walipindua meza kibabe kupitia kwa Abdoulaye Doucoure dakika ya 49, James Rodriguez dakika ya 52 na msumari wa kuweka mzani sawa ulipigiliwa dakika ya 90+5 na Dominic Calvert-Lewin.

Matokeo hayo yanaifanya United ifikishe pointi 45 ikiwa nafasi ya pili baada ya kucheza mechi 23 huku Everton ikiwa nafasi ya sita na pointi 37 baada ya kucheza mechi 21.

Ole amesema: "Tumecheza vizuri na viwango kwa wachezaji vikizidi kuimarika ila ninadhani kwamba kwa wakati huu hatuna hesabu kubwa za kutwaa ubingwa tunaweka nguvu kubwa kujiimarisha zaidi".

# Werner atarudia ubora - Tuchel

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesisitiza Timo Werner "ainaimarika kila siku" licha ya raia huyo wa Ujerumani kutofunga katika mechi 14 za Ligi Kuu England.

Werner aliwasili Stamford Bridge akitarajiwa kuwa mfungaji mzuri zaidi akitokea kwenye timu ya Ligi Kuu Ujerumani, RB Leipzig, kuelekea kuanza kwa msimu wa 2020-21.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amefunga mabao manne tu katika mechi 22 za Ligi Kuu, huku pia akishindwa kufunga Jumapili wakati Chelsea ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Sheffield United.

Huo ulikuwa ni ushindi wa tatu mfululizo kwa kocha Tuchel tangu achukue mikoba ya kuinoa Chelsea baada ya kufukuzwa kwa Frank Lamaprd.

Pamoja na Werner kutopata nafasi ya kufunga, Tuchel bado hana shaka na mshambuliaji huyo, kwani anaamini mambo yatabadilika tu.

"Alicheza vizuri, lakini hakufunga, sina shaka naamini atarudi tu katika ubora wake unaotakiwa," alisema kocha wa zamani, Paris Saint-Germain.



# Klopp amtaja Alisson kipigo Liver

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp ameona ishara chanya kwa Liverpool, lakini akikiri "makosa mawili makubwa" yaliyofanywa na Alisson yaliwafanya wakachapwa 4-1 na Manchester City.

Bingwa huyo mtetezi wa Ligi Kuu alikutana na kipigo cha tatu mfululizo na kuwaacha wakiwa nje ya mbio za ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu.

City sasa ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi sita zaidi dhidi ya Manchester United, lakini wamewapita Liverpool kwa pointi 10, huku kikosi cha Pep Guardiola kikiwa na mchezo mmoja mkononi.

Bao la kuongoza la Ilkay Gundogan kipindi cha pili lilisawazishwa kwa penalti na Mohamed Salah pale kwenye dimba la Anfield, lakini makosa mawili ya Alisson yakaisaidia City kupata ushindi wa 14 mfululizo kwenye mashindano yote.

"Unapopoteza kwa mabao 4-1 si siku yako. Sehemu kubwa ya mchezo ilikuwa nzuri na kikosi changu kilicheza vizuri, kwa uhakika tulicheza soka zuri," alisema Klopp akiiambia Sky Sports.

"Kipindi cha kwanza tulicheza soka la kuvutia, lakini baadaye City walibadilisha mfumo na wakawa wanacheza 4-4-2 na mambo yakabadilika kuanzia hapo.

"Ilikuwa ngumu na sisi kuzoea mfumo wao haraka na mwanzoni hatukuweza kuwa katika kile kiwango kinachotakiwa na tukakosa nafasi nyingi za wazi."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE ATOA NENO NEYMAR KUBAKI PSG

● ● ● Ni habari kubwa, kila mmoja anajua alivyomuhimu kwetu, natumai anaweza kuandika historia kwa...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amekaribisha kauli ya Neymar kuhusu majaliwa yake pale Paris Saint-Germain, akisema mchezaji mwenzake huyo anastahili kufurahia historia ya mafanikio nchini Ufaransa.

Neymar, ambaye mara kadhaa amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka PSG tangu alipojiunga na miamba hao wa Ligue 1 mwaka 2017, mwezi uliopita alionyesha ishara ya kutaka kubaki jijini Paris.

Nyota huyo wa Brazil aliiambia TF1: "Nataka kubakia PSG na natumai Kylian atabaki pia."

Neymar ameripotiwa kukaribia kusaini mkataba wa miaka minne na klabu hiyo na alikuwa nguzo muhimu kwenye mchezo wa Jumapili wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Marseille licha ya mapema wiki hii kuwa mgonjwa.

Kuwabakiza Neymar na Mbappe bodi ya klabu hiyo itakuwa imeipa nguvu zaidi PSG katika nia yake ya kushinda taji la Lgi ya Mabingwa Ulaya, wakiwa wamefika fainali chini ya kocha, Thomas Tuchel msimu uliopita.

Na Mbappe aliiambia Canal+ kuhusu maoni yake juu ya Neymar.

"Ni habari kubwa. Kila mmoja anajua jinsi alivyomuhimu kwetu," alisema mshindi huyo wa Kombe la Dunia.

"Natumai anaweza kuandika historia kwa Paris kwa kipindi kirefu kijacho. Yeye na klabu wanastahli hilo."

Mbappe alikuwa akizungumza baada ya kufunga bao la ufunguzi dhidi ya Marseille, alilotupia dakika ya tisa ya mchezo huo.

Hakuna mchezaji wa PSG amecheza mechi nyingi (26) au kufunga mabao zaidi (18) katika mashindano yote kuliko Mbappe msimu huu, akipitwa na Angel Di Maria pekee kwenye pasi za mwisho.

Mauro Icardi, ambaye kwa sasa ana mabao matano kwenye ligi katika mechi 11, aliongeza la pili katika ushindi huo wa juzi.

## KWA UFUPI

**MOURINHO ATAKA SUBIRA SON**

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, anaamini ni jambo la "kusubiri muda muafaka" linapokuja suala la kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na straika wa Korea Kusini, Son Heung-min mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2023. ***(Evening Standard)***

**JAMBO LA RAMOS BADO**

KUUMIA kwa mlinzi wa Hispania, Sergio Ramos, kunaweza kushuhudia mazungumzo ya mkataba mpya yakisimama kwa muda, hadi kupona kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34. ***(Marca)***

**HODGSON NA OFA YA ZAHA**

KOCHA wa Crystal Palace, Roy, anatarajia kupata ofa kwa ajili ya winga wake, Wilfried Zaha kipindi cha majira ya joto, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, malengo yake ni kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

**PIOLI AMFURAHIA IBRAHIMOVIC**

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli, amesema ni jambo la "heri" kuona straika wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic, anaendelea kuichezea timu hiyo ya Italia. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, unamalizika kipindi cha majira ya joto na miamba hao wa Serie A. ***(Sky Sports Italia, via Football Italia)***

**OVERMARS KUONDOKA AJAX**

MKURUGENZI wa Soka wa Ajax, Marc Overmars, anapanga kuondoka kwenye nafasi yake hiyo mwishoni mwa msimu huu, huku nyota huyo wa zamani wa Uholanzi akitajwa kutaka kujiunga na timu yake ya zamani ya Barcelona au Arsenal. ***(Mundo Deportivo)***

**NDOMBELE KUBADILIKA**

KIUNGO wa Ufaransa, Tanguy Ndombele, mwenye umri wa miaka 24, amebainisha kwamba anatakiwa kubadilika kama anataka kufanikiwa na Tottenham kwenye Ligi Kuu. ***(Telegraph)***

**WERNER ATAKA MABAO**

STRAIKA wa Chelsea na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 24, hajafunga bao katika mechi 14 za Ligi Kuu England, lakini amesema kwamba, ataendelea kujituma na mabao yatakuja. ***(Evening Standard)***

**GREALISH KUONGEZWA MSHAHARA**

ASTON Villa wapo tayari kumpa ofa ya mshahara mkubwa, Jack Grealish na kumbakiza Ross Barkley pale Villa Park. Klabu hiyo ipo tayari kumpa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki ili abakie klabu hapo na wataikataa ada ya Chelsea ya pauni 40 ya kumnunua Barkley.***(Sky)***

**HENDRY KUTUA JUMLA OOSTENDE**

NYOTA wa Celtic, mwenye umri wa miaka 25, Jack Hendry, anatarajia kujiunga moja kwa moja kutoka na Oostende ya Ubelgiji kutoka usajili wake wa sasa wa mkopo.***(BBC Sport)***

**MOYES AMTAKA ARMSTRONG**

DAVID Moyes anataka West Ham imfuatilie mshambuliaji wa Blackburn, Adam Armstrong mwenye umri wa miaka 23, ili wamsajili kipindi cha majira ya joto.***(Mail)***

**SOLSKJAER AKOMAA NA POGBA**

OLE Gunnar Solskjaer amesema bado anaendelea kuzungumza na kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, kuhusu majaliwa yake. Pogba mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka hapo Old Trafford. ***(Sky)***

HABARI MICHEZO

# SIMBA KINARA KUKOSA PENALTI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

CLATOUS Chama, kiungo mshambuliaji raia wa Zambia, ameiingiza Simba kwenye rekodi ya kuwa timu inayoongoza kwa kukosa mikwaju ya penalti mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Jumapili iliyopita, Chama alikosa mkwaju wa penalti, kipindi cha kwanza ambayo ilipanguliwa kwa ustadi na kipa Mganda Mathias Kigonya wa Azam FC, aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Zambia kabla ya kusajiliwa na 'Wanalambalamba' hao kipindi cha dirisha dogo.

Ni penalti ambayo ingeweza kuipa ushindi Simba, lakini mechi ikaisha kwa sare ya mabao 2-2.

Hadi sasa Simba inakuwa imekosa penalti mara mbili msimu huu na hakuna timu yoyote iliyokosa kwa idadi hiyo.

Penalti ya kwanza ilipotezwa na nahodha wa timu hiyo, John Bocco Oktoba 26, Simba ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Mpaka sasa mabingwa hao watetezi wamebahatika kuzawadiwa jumla ya penalti nne, mbili ikikosa na mbili ikishinda.

Bocco alifunga penalti kwenye mechi ambayo Simba iliichapa Kagera Sugar mabao 2-0 Novemba 4, kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam na Meddie Kagere alipachika penalti Desemba 16, mwaka jana, likiwa ni bao pekee, Simba ikishinda 1-0 dhidi ya KMC.

Jumla ya penalti 25 zimeshapatikana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara haki sasa, 17 zikiwekwa kimiani na nane zikiota mbawa kwa kutoka nje, au makipa kuokoa.

NI HUYU HAPA...



Mshindi wa nafasi ya Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, akipongezwa na baadhi ya wanachama wa klabu hiyo, huku vyombo vya habari navyo vikitumia fursa hiyo kupata maoni yake baada ya kumbwaga mpinzani wake, Juma Nkamia, katika uchaguzi huo uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Filamu ya Binti kushiriki Tamasha la 29 la PAFF

**Na Mwandishi Wetu**

FILAMU ya Kitanzania iitwayo 'Binti' imechaguliwa kushiriki katika Tamasha la 29 la Filamu la Pan Afrika (PAFF), litakalofanyika Machi 8, mwaka huu jijini Los Angeles, Marekani.

Akizungumza na waandishi wa habari, mwongozaji wa filamu hiyo, Seko Shamte, alisema kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, tamasha hilo litaonyeshwa kwa njia ya mtandao Machi 8, mwaka huu.

Seko alisema: "Katika majiji ya Afrika Mashariki likiwamo Dar es Salaam ambapo filamu hiyo imetengenezwa, wananchi watapata wasaha wa kuiona itakavyokuwa ikioneshwa kwenye tamasha hilo katika jiji hilo".

Seko ambaye aliwahi kutamba na Filamu ya 'Home Coming', alisema katika uandaaji wa filamu hiyo ameshirikiana na ndugu wawili Angela na Alinda Ruhinda wa Kampuni ya Black Unicorn Studios, na itakuwa ikisambazwa na Okado Media.

Alisema wahusika wakubwa katika filamu hiyo ni Angela na Alinda, huku ikihusu maisha ya mabinti waishio mjini na namna ambavyo wanahangaika kuendesha maisha yao.

Seko alisema wahusika hao ni mara yao ya kwanza kuigiza, lakini wameonyesha uwezo mkubwa katika uigizaji.

Naye Alinda Ruhinda, alisema filamu hiyo inahusu maisha ya mabinti, lakini inafaa kutazamwa na watu wote na kwamba itafungua milango kwa watayarishaji wa filamu mbalimbali hapa nchini.

Kwa upande wa mmiliki mwenza wa kampuni hiyo, Angela Ruhinda, alisema ni muda muafaka kwa Tanzania kujitangaza kimataifa katika sekta ya filamu kupitia filamu hiyo kwa sababu kuna mazingira mazuri ya kuigizia.

## Mafunzo kusajili wa3 ikisaka ubingwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa timu ya Mafunzo inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Abdallah Bakar 'Edo', amesema kuelekea usajili wa dirisha dogo msimu huu, anatarajia kusajili wachezaji watatu ambao anaamini wataisaidia timu kutwaa ubingwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo, alisema anatarajia kufanya usajili kwenye nafasi tatu ambazo anaona ni muhimu katika kukiongeza nguvu kikosi chake kwa sasa.

Alitaja nafasi hizo kuwa ni mshambuliaji mmoja, beki wa pembeni pamoja na kiungo wa chini (namba sita), huku akifafanua kuwa idara hizo ndio tatizo katika kikosi chake kwa sasa.

"Kwa sasa ni mapema kuweka wazi wachezaji hao wanatoka timu gani, ila tupo katika mazungumzo wakati huu tukisubiri dirisha lifunguliwe ndio tuweke wazi kupitia vyombo vya habari, lakini wachezaji ambao tumepanga kuwasajili wanauwezo unaohitajika na kikosi changu," alisema.

Aidha, akizungumzia mchezo wake wa jana wa kukamilisha mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo ambao alipata ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya mabingwa watetezi, Mlandege FC, alisema wachezaji waliuanza ari kubwa lengo likiwa ni kuhakikisha wanapata ushindi.

## Kilimani City kugeukia mbeleko ya mashabiki

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kilimani City FC, imesema itaendelea na mbinu ya kuhamasisha mashabiki wake kwenda uwanjani kwa wingi pindi ikicheza ili kutoa hamasa kwa wachezaji wake kufanya vizuri.

Hayo yameelezwa na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nassor Salum, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu mbinu wanazopaswa kutumia ili kuongeza morali kwa wachezaji wao.

Alisema timu hiyo katika michezo mitatu mfululizo imefanya vizuri kwa kutoka na ushindi hali inayosababisha mashabiki kuendelea kumiminika kila inaposhuka dimbani.

"Hamasa ya mashabiki kwa kiasi fulani inachangia hata wachezaji kufanya vizuri, kwani huwatia moyo wa kucheza kwa ari," alisema.

Aidha, akizungumzia kuhusu timu hiyo kupata kadi nyingi za onyo uwanjani, alikubali kuwa hali hiyo inaweza kuwagharimu wakati watakapokuwa wakikabiliwa na mechi ngumu.

Hata hivyo, alisema tatizo hilo la Kadi atalifanyia kazi kwa kukaa na kikosi chake Ili kuwapa darasa la nidhamu mchezoni jambo litakalosaidia kujiepusha na kadi zisizo za lazima.

Michezo

Jumanne Februari 9, 2021

Nipashe



MBAPPE ATOA NENO NEYMAR KUBAKI PSG HABARI UK 22

# KAZE APIKA MABAO YA FISTON, SARPONG YANGA

## ●●●Atahadharisha dhidi ya Mbeya City Jumamosi huku akieleza kila mechi sasa wanapaswa kuichukulia kama...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema anaifungia kazi safu ya ushambuliaji ya timu hiyo, ili kuhakikisha inakuwa makini na kuongeza umakini katika kutumia vizuri nafasi wanazotengeneza uwanjani.

Safu ya ushambuliaji ya Yanga ambayo imekuwa ikiongozwa na Mghana Michael Sarpong, wiki iliyopita wakati wakilala kwa bao 1-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya African Sports ya Tanga, ilikuwa chini ya usajili mpya wa dirisha dogo, Mrundi Fiston Abdoulrazak, lakini ikashindwa kuambulia kitu nyavuni, jambo ambalo limemwamsha Kaze.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaze alisema walitengenezeza nafasi nyingi katika mechi hiyo ya kirafiki, lakini walikosa utulivu na kushindwa kuzitumia ipasavyo.

Alisema wameanza kufanyia kazi safu ya ushambuliaji, ikiwamo kwa kuongeza umakini katika kumalizia nafasi wanazotengeneza kwa kuwa kila mchezo kwenye raundi hii ya pili ya Ligi Kuu Bara, kwao ni fainali na wanahitaji kupata matokeo chanya.

"Kila mchezaji anajua majukumu yake akiwa ndani ya uwanja, ninawaamini vijana wangu wanafanya kazi vizuri, muhimu kwetu ni kushinda, ushindi utapatikana kwa kuongeza umakini na utulivu kwa nafasi tunazozitengeneza.

"Hakuna mechi rahisi kwa sasa kila timu inahitaji kupata pointi, tunaangalia maandalizi yetu pamoja na nguvu kubwa kwenye kusaka ushindi ndani ya dakika 90," alisema Kaze.

Kuelekea mechi ya Jumamosi dhidi ya Mbeya City itakayopigwa katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Kaze alisema, wapinzani wao hao ni timu nzuri na imeimarisha kikosi chake, lakini hilo halina shaka kwa sababu nao pia wameongeza watu ndani ya kikosi chao, ila hawataingia uwanjani kwa kujiamini kwa asilimia zote kwa kuwa wenyeji wao hawako katika nafasi nzuri kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 msimu huu.

Naye kocha wa viungo wa Yanga, Edem Mortotsi, alisema wamekuwa na utaratibu kwa wachezaji wanaocheza dakika chache katika mechi kuwabakisha uwanjani kuendelea na mazoezi baada ya mchezo kumalizika ili kuwaweka fiti.

Alisema hakuukuta utaratibu huo, ila ameuanzisha ili kuwafanya wachezaji wote wanaokuwapo kwenye mipango ya mchezo miili yao iwe fiti kwa mechi licha ya kukosa dakika 90.

"Ni vizuri wachezaji walikuwapo kwenye mipango ya mechi siku hiyo, kila mmoja awe amecheza takribani dakika 50 na kuendelea, kwa wale wanaoingia na kucheza dakika 10 au 20, wanalazimika kubaki uwanjani kuendelea na mazoezi, baada ya dakika 90 za mchezo kumalizika," alisema Mortotsi.

Yanga bado inaendelea kushikilia usukani wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 44 baada ya kucheza mechi 18 bila kupoteza huku ikitoka sare tano, wakati huu Simba ambayo ina kiporo kimoja mkononi, ikiwa nafasi ya pili na alama zake 39.

Baada ya mechi hiyo dhidi ya Mbeya City, Yanga itarejea Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuikaribisha Kagera Sugar Februari 17, kabla ya siku tatu baadaye kuialika Mtibwa Sugar uwanjani hapo.

## TUTA HILO...



Beki wa kati wa Manchester City, Ruben Dias (kushoto), akimchezea madhambi mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, ambayo yalisababisha penalti iliyofungwa na straika huyo kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi na Man City kushinda 4-1. **PICHA: MTANDAO**

## SIMBA YAGEUZIA MITUTU AS VITA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikilazimishwa sare katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Azam FC juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Dider Gomes, amesema hawezi kuwabebesha lawama wachezaji wake kwa kushindwa kupata pointi tatu na badala yake sasa amewataka kuelekeza akili zao dhidi ya AS Vita ya DR Congo.

Simba ambayo mbali na Wakongo hao kwenye Kundi lao la A ipo pamoja na Al Ahly ya Misri na Al-Merrikh ya Sudan, itashuka uwanjani mjini Lubumbashi, DR Congo Ijumaa wiki hii dhidi ya AS Vita kwenye mechi ya kwanza ya hatua ya makundi.

Akizungumza na Nipashe jana, Gomes alisema wachezaji wake walipambana dhidi ya Azam FC, ila tatizo ni moja tu, walishindwa kutumia nafasi walizotengeneza katika mchezo wao huo wa kiporo cha Ligi Kuu.

Gomes alisema mchezo ulikuwa mzuri na wa ushindani mkubwa kwa kila timu kugawana vipindi, wachezaji wake wakimiliki dakika 45 za kipindi cha kwanza, lakini wakashindwa kumaliza mchezo mapema kwa kutumia nafasi walizozitengeneza ikiwamo kiungo Clatous Chama kukosa mkwaju wa penalti.

"Ilikuwa mechi ya ushindani mkubwa, tulimiliki mpira kipindi cha kwanza, wapinzani wetu wakafanya mabadiliko na kutumia upungufu wetu ikiwamo kati na kufanikiwa kupata pointi mmoja.

"Sasa tunasahau matokeo ya mechi ya jana (juzi), na tunaenda kufanyia kazi upungufu wetu ili kujiimarisha kwa mechi yetu dhidi ya AS Vita, ninaimani na wachezaji wangu kufanya vizuri katika mchezo huo wa Ligi ya Magingwa tutakaocheza Ijumaa hii DR Congo," alisema Gomes huku akifafanua kuwa kikosi hicho kinatarajia kuondoka leo jijini Dar es Salaam kuelekea DR Congo tayari kwa mechi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002